**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**
**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

# HOTUBA YA BAJETI YA KAIMU WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE

**MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM),**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 AKIWASILISHA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**MEI, 2026.**



**Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi**
**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

# YALIYOMO

A. UTANGULIZI ........................................................1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA..........................3
C. MAPATO YALIYOKUSANYWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025-MACHI 2026)..................5
D. MAFANIKIO YA WIZARA ..............................................6
SEKTA YA UTALII ........................................................6
SEKTA YA MAMBO YA KALE........................................13
E. CHANGAMOTO ZA WIZARA NA UTATUZI WAKE ...........16
F. FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025-MACHI 2026)..........................................18
G. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE ...............................................................20
H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026...............................................21
I. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2025-MACHI 2026 .................28
I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE. ...28
UTEKELEZAJI HALISI32
II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII ...34
UTEKELEZAJI HALISI...................................................35
III.PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII ...............................................................40
UTEKELEZAJI HALISI...................................................40

IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII .... 42
UTEKELEZAJI HALISI ............................................... 43
V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE .................... 46
UTEKELEZAJI HALISI ............................................... 47
UTEKELEZAJI HALISI ............................................... 50
UTEKELEZAJI HALISI ............................................... 52
J. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027 . 55
K. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027................................................................ 57
L. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027................................................... 59
M. SHUKURANI .......................................................... 71
N. HITIMISHO ............................................................ 76
VIAMBATISHO ........................................................... 78

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AFD | Agence Francaise de Developpement |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| EU | European Union |
| GSTC | Global Sustainable Tourism Council |
| HAZ | Hotels Association of Zanzibar |
| ITB | International Tourism Board |
| IPA | Institute of Public Administration |
| IT | Information Technology |
| JIKA | Japan International Cooperation Agency |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| KVZ | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| NMB | National Microfinance Bank |
| NACTIVET | The National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| PBZ | Peoples Bank of Zanzibar |
| PDB | Presidential Delivery Bureau |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| SMT | Serikali ya Muungano Tanzania |
| SUZA | The State University of Zanzibar |
| TANAPA | Tanzania National Parks Authority |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TBI | Tony Blair Institute |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UAE | United Arab Emirates |
| UNIDO | United Nations Industrial Development Organization |
| UNECA | United Nations Economic Commission for Africa |

| | |
|---|---|
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| UNCDF | United Nations Capital Development Fund |
| UNICEF | United Nations International Children’s Emergency Fund |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| USAID | United States Agency for International Development |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| ZATI | Zanzibar Association for Tourism Investors |
| ZATO | Zanzibar Association of Tour Operators |
| ZATOGA | Zanzibar Tour Guide Association |
| ZIToD | Zanzibar Institute of Tourism Development |
| ZITF | Zanzibar International Trade Fair |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund |

# HOTUBA YA BAJETI YA KAIMU WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE, MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA 2026/2027, AKIWASILISHA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutupa neema ya uzima na uhai na kutuwezesha kukutana tena leo, ili tuweze kujadili Makadirio na Matumizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Aidha, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa Amani na utulivu katika nchi yetu, tunamuomba Mwenyezi Mungu atudumishie Amani hii.

2. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo kwa mara nyengine katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 ili kuendelea kuiongoza Zanzibar. Matokeo hayo yametokana na Maendeleo Makubwa ambayo ameyafanya ambayo yamewagusa wananchi wote wa visiwa vya Unguja na Pemba. Vile vile niendelee kumpongeza kwa kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 – 2025 na kupindukia shabaha ya utekelezaji wake. Aidha, naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeikiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi kubwa ambazo amezionesha za kuutangaza utalii wetu ndani na nje ya nchi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuongoze katika kipindi chake cha pili cha uongozi wake ili aendelee kutuongoza na kutufikisha katika mafanikio yake mengine makubwa zaidi ambayo yamepangwa kwa wananchi wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uwezo, nguvu, hikma, busara na bidii ya kuiongoza nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kushinda kwa ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2025. Ushindi huu unatokana na kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuwaletea mapinduzi ya kiuchumi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, naomba nimpongeze kwa juhudi kubwa anazozichukuwa za kuitangaza nchi kitaifa, kikanda na Kimataifa na hususan katika Sekta hii ya Utalii. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima, busara, afya, pamoja na kumuongoza ili aweze kuendelea kuitumikia nchi yetu kwa uaminifu na uadilifu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako naomba nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kuteuliwa tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais na hii ni kutokana na utendaji wake wa kazi ulioimarika wa kuwaletea wananchi maendeleo ya haraka ambao umepelekea Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali

Mwinyi, kumuamini tena na kumpa nafasi ya kuendelea kuwa msaidizi wake, ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha pili cha mwaka 2025 – 2030. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuwezeshe na amuongoze ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa udhati kabisa, naomba nichukue nafasi hii adhimu, kuwapongeza nyote kwa kuchaguliwa na kuaminiwa na wananchi kuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Pia naomba nikupongeze kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Tunatumai utaliongoza vyema Baraza hili kwa kipindi cha miaka hii mitano.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo Mheshimiwa Fatma Ramadhan Mandoba pamoja na wajumbe wote wa Kamati hii. Naamini kuwa mawazo, maelekezo, maagizo na miongozo ambayo wanatupatia tutaendelea kuyafanyia kazi kwa lengo la kuendeleza maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imeundwa kwa lengo la kusimamia sekta kuu mbili ambazo ni Utalii na Urithi wa Mambo ya Kale. Vile vile, Wizara hii imepewa majukumu ambayo huyatumia katika kupanga malengo ya Idara na Taasisi zake.

## MUUNDO WA WIZARA

**8.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inasimamia Idara na taasisi zifuatazo: -

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
iii. Idara ya Utalii
iv. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
v. Kamisheni ya Utalii
vi. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe
vii. Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar (ZITOD)
viii. Ofisi Kuu Pemba

## MAJUKUMU YA WIZARA

**9.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine, inatekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kusimamia Sheria, Sera, Mipango, Tafiti na Mikakati ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.
ii. Kuimarisha Utalii Endelevu na kwa Wote unaojali mazingira, silka na utamaduni wa visiwa vyetu.
iii. Kutoa elimu na uelewa kuhusu Utalii Endelevu ikiwemo uendelezaji wa ubunifu na ujasiriamali katika utalii kwa kusaidia upatikanaji wa nyenzo, mitaji na masoko ya ndani na nje.
iv. Kuimarisha mazao mbali mbali ya Sekta ya Utalii ikiwemo Utalii wa Fukwe na Bahari, Utalii wa Michezo, Utalii wa Mikutano, Utalii wa Afya, Utalii wa Vyakula,

Utalii wa Sanaa na Utamaduni, Utalii Halal, Utalii wa Urithi wa Mambo ya Kale.

v. Kukuza pato la nchi kupitia Sekta ya Utalii na Urithi wa Mambo ya Kale kwa kuimarisha minyororo ya thamani na mifumo ya ugavi kwa mashirikiano na sekta binfasi na wadau wa maendeleo.

vi. Kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi na kuvutia uwekezaji zaidi kwa mashirikiano na wadau wa maendeleo na sekta binafsi.

vii. Uwezeshaji wa wananchi katika ujasiriamali na ajira kupitia programu na miradi ya kiutalii itakayotoa tija.

viii. Kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza Makumbusho ya kale na ya kisasa ndani ya Zanzibar.

ix. Kuyalinda, kuyakarabati, kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

x. Utunzaji wa vitu na mabaki ya kihistoria ili kuweka kumbukumbu kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

xi. Kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar.

xii. Usimamizi na Uendelezaji wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii ili kiweze kutoa huduma bora zinazoendana na viwango vya kimataifa.

## C. MAPATO YALIYOKUSANYWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025-MACHI 2026)

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika mwaka wa fedha 2025/2026 ilipangiwa kukusanya **Shilingi 2,250,000,000/=.** Hadi kufikia

Machi 2026 Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 1,272,438,373/=** sawa na asilimia **57**.

Aidha, kupitia Kamisheni ya Utalii ambayo mapato yake hutumia kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Sekta ya Utalii ikiwemo ukusanyaji wa mapato yanayotokana na shughuli za utalii pamoja na uendeshaji wa ofisi, ilipanga kukusanya **Shilingi 11,668,715,869/=** na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 10,522,670,379.38/=** sawa na asilimia 90.

Vile vile, kwa Upande wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ilipanga kukusanya **Shilingi 3,600,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 2,287,677,102/=** sawa na asilimia **63.5 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1A)**

## D. MAFANIKIO YA WIZARA

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Wizara imefanikiwa kufanya yafuatayo:-

## SEKTA YA UTALII

i. **Kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini**
Kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi, kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watalii wanaoingia nchini. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia hapa nchini mwaka 2025 kwa asilimia 24.5 kutoka watalii

736,755 mwaka 2024 hadi kufikia watalii 917,167 mwaka 2025.

ii. **Kuongezeka kwa siku za ukaazi kwa mtalii**

Kutokana na ongezeko la vivutio zaidi vya utalii ambavyo vinaimarishwa na kuibuliwa imepelekea kuongezeka kwa wastani wa siku za ukaazi kwa wageni. Kufikia mwaka 2024, mgeni mmoja hutumia wastani wa siku nane kulinganisha na wastani wa siku saba kwa kila mgeni katika Mwaka 2022. Kuongezeka kwa ukaazi huu kwa wageni kumetokana na juhudi za Serikali ambazo zimefanywa za kuimarishwa kwa miundombinu mbali mbali ya mnyororo wa thamani wa Sekta ya Utalii ikiwemo ongezeko la hoteli za madaraja ya juu, ongezeko la vyumba vya hadhi ya juu, viwanja vya ndege, barabara, bandari, huduma za makaazi na ulazi ikiwemo hoteli za hadhi ya juu pamoja na nyumba za kulala wageni zenye viwango vya kimataifa, huduma za ukarimu na ushirikishwaji wa moja kwa moja wa wananchi katika kuibua na kuongeza vivutio vya Utalii vilivyopo nchini.

iii. **Zanzibar kushinda na kutunukiwa heshima tofauti za Utalii duniani**

Zanzibar imekuwa ikirishiriki katika matukio ya kimataifa ambayo hujishughulisha na utoaji wa tunzo mbali mbali za utalii kwa nchi au kisiwa kinachofanya vizuri zaidi ya visiwa vyengine. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2025/2026 Zanzibar imefanikiwa kupata tunzo ya "Africa Corporate Retreat Destination". Kupatikana kwa tunzo hio kumepelekea kuitangaza zaidi Zanzibar kitaifa, kikanda na kimataifa na kupelekea kuongezeka kwa idadi ya watalii

wanaokuja kutembelea nchini. Zanzibar pia imetambulika kuwa miongoni mwa vivutio vikuu barani Afrika vinavyoongoza katika ubora wa huduma za viwanja vya ndege, idadi ya mashirika ya ndege za kimataifa zinazoleta watalii na ongezeko la idadi ya uwekezaji wa hoteli za hadhi ya juu kwa mwaka.

**iv. Kushiriki katika Matamasha Yanayotangaza Vivutio vya Utalii Zanzibar**

Wizara inaendelea kushiriki kikamilifu katika matamasha, maonesho na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi yanayolenga kuitangaza Zanzibar pamoja na vivutio vya utalii vilivyopo. Miongoni mwa matamasha hayo ni pamoja na Tamasha la Oman – Zanzibar Cultural Week, Siku ya Mji Mkongwe, Siku ya Makumbusho, pamoja na mashindano ya michezo na utamaduni. Vile vile, Wizara ilishiriki maonesho ya kimataifa ambayo ni World Travel Market (WTM) London, ITB Berlin, WTM Africa (Cape Town), na kwa upande wa maonesho ya Kikanda Wizara ilishiriki katika maonesho ya Karibu-Kilifair (Arusha) na Swahili International Tourism Expo (SITE).

Tayari Zanzibar inatarajiwa kuwa mwenyeji wa maonesho ya kimataifa ya ITOP mwaka 2027 pamoja na jukwaa la World Travel Market (WTM). Halikadhalika, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kuwa miongoni mwa viongozi wakuu wa kimataifa watakaoshiriki katika Maonesho ya Utalii wa Visiwa Kimataifa (World Island Exhibition) na ITOP itakayofanyika nchini Korea Kusini,

mwezi wa Oktoba 2026.

Ushiriki katika matamasha haya umechangia kwa kiasi kikubwa kuitangaza Zanzibar Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, kuimarisha ushirikiano na wadau wa sekta ya utalii, na hatimaye kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini.

**v. Kukua kwa vivutio zaidi vya utalii.**

**a) Utalii wa Michezo:**

Kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuongeza matukio ya kuwavutia watalii nchini, kumepelekea kukuwa kwa vivutio mbali mbali vya utalii ikiwemo utalii wa michezo hususan mashindano ya CHAN ya mwaka 2026, na matayarisho kuelekea katika mashindano ya AFCON 2027. Miongoni mwa michezo mengine maarufu ni kama vile mashindano ya vishada vya bahari (kite surfing), mbio za riadha kama "Marathon" na"Triathlon", mashindano ya mpira wa ufukweni yaani "Beach Soccer," na mashindano ya michezo ya "Beach Volleyball".

**b)Utalii wa Mikutano:**

Zanzibar imeendelea kuimarisha na kuvutia zaidi utalii wa mikutano ya kikanda na kimataifa. Mikutano mikubwa kama AVIADEV, Zanzibar Investment Summit, Zanzibar Tourism Summit, Mikutano ya Umoja wa Afrika, Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia, imefana sana katika kuinyanyua sekta hii ya Mikutano ya Kimataifa inayofanyika Zanzibar. Mwakani itakuwa mwenyeji wa Jukwaa la ITOP.

## c) Utalii wa Halal:

Zanzibar imeendelea kuimarisha na kuvutia zaidi utalii wa Halal ikiwemo mashindano ya kimataifa ya kuhifadhi Qur-an, mikutano ya kiimani kama vile ya Mufti Menk, Utalii wa urithi wa utamaduni wa kiislamu. Vile vile, Zanzibar imeendelea kuimarisha mahusiano ya tamaduni za pwani katika bahari ya hindi na inashirikiana na nchi kama Oman na Qatar katika kuhuisha utalii wa kizuoni na imefana sana katika kuinyanyua sekta hii ya Mikutano ya Kimataifa inayofanyika Zanzibar.

## d) Utalii wa Sanaa na Utamaduni:

Zanzibar imeendelea kuimarisha urithi wa utamaduni wake ikiwemo kukondoisha matumizi ya lugha ya kiswahili, kuendeleza vivutio asilia vya utalii wa urithi unaoshikika na usioshikika. Mwaka 2026 Zanzibar itakuwa mwenyeji wa Siku ya Utamaduni wa Kimataifa ya UNESCO.

## e) Utalii wa Vyakula Asilia:

Utangazaji wa utamaduni wa mapishi ya vyakula asilia vya Zanzibar umeongezeka sana katika kipindi hiki cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane. Watalii kutoka maeneo mbali mbali ulimwenguni wamekuwa wakija Zanzibar kujionea na kujifunza mapishi mbali mbali ya utalii wa vyakula vya mwambao wa Afrika mashariki na kukuza hazina hii ya urithi usioshikika unaowajali sana wananchi wa kawaida.

### f) Utalii wa Meli:

Utalii wa meli ni moja ya eneo linaloendelea kuimarika na kuchangia kuimarisha sekta ya utalii hapa Zanzibar kwa kuwa kituo kinachochipukia kwa nguvu kwa utalii wa meli 'Cruise tourism'. Idadi ya meli za kitalii zinazotembelea nchini na zilizopanga ratiba ya kutembelea Zanzibar imeongezeka ambapo kwa kipindi cha 2023 hadi 2026 jumla ya kampuni 27 za meli zilileta meli zake Zanzibar ambapo zilifunga nanga Unguja mara 37 na Pemba mara 31. Meli hizo hutembelea Zanzibar na kushusha watalii wengi ambao hupata fursa ya kuvitembelea vivutio mbali mbali vya kitalii ikiwemo mashamba ya viungo, msitu wa Jozani na maeneo ya Mji Mkongwe na kununua bidhaa za zawadi katika maeneo wanayotembelea. Aidha misafara ya meli 13 imethibitishwa kuja Zanzibar kwa mwaka huu wa 2026.

### g) Utalii wa Mambo ya Kale:

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, pamoja na kuimarisha makumbusho, maeneo ya kihistoria, utafiti wa kiakiolojia, imeongeza matamasha na maadhimisho mbali mbali ya urithi wa historia yetu na mambo ya kale kama vile kuadhimisha Siku ya Upigwaji Marufuku Biashara ya Utumwa, Siku ya Makumbusho Duniani, Siku ya Urithi Duniani, Siku ya Mji Mkongwe, Wizara katika mwaka huu wa 2026 inashirikiana na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka katika kuadhimisha Siku ya Kumbukumbu na Nyaraka Duniani.

### vi. Kutangaza utalii ndani na nje ya nchi.

Katika kuhakikisha Zanzibar inazidi kutangaza vivutio vyake kimataifa, Kamisheni ya Utalii inatekeleza mikakati ya kuitangaza Zanzibar katika soko kubwa la utalii duniani lililopo nchini Uingereza, kwa kutumia matangazo ya mabasi maarufu ya Mji huo yanayofanya safari zake katika jiji la London. Kuwekwa kwa matangazo hayo kutapelekea kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini.

### vii. Kuimarika kwa Mfumo wa Upimaji wa Pato la Taifa katika Sekta ya Utalii (Tourism Satellite Account)

Katika kuimarisha takwimu sahihi zinazotoa mafanikio ya maendeleo ya utalii hapa Zanzibar, Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Uchumi Barani Afrika (UNECA) imeandaa mfumo wa Upimaji wa Mchango wa Utalii kwenye Pato la Taifa (Tourism Satellite Account). Kwa sasa wataalamu kutoka UNECA wameshatoa mafunzo kwa maafisa pamoja na wadau wa Sekta ya utalii ili kuweza kukamilisha taarifa mpya za pato la taifa katika sekta ya utalii. Kukamilika kwa zoezi hili kutapelekea kuwa na takwimu sahihi za ongezeko la mchango wa taifa wa utalii kupita takwimu za sasa za asilimia 29.2 katika pato la Taifa.

### viii. Elimu na Uwezeshaji wa Wanajamii katika Ujasiriamali na Ajira

Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo imeongeza mawanda yake ya kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na uimarishaji wa ufanisi wao katika kutoa huduma mbali mbali za ukarimu katika sekta zao makhsusi kuhusu utalii endelevu ikiwemo wanajamii kutoka Unguja na Pemba kama vile watembeza watalii, watengeneza misafara ya utalii, wamiliki wa mahoteli, wasimamizi wa huduma za ukarimu na malazi, pamoja na wajasiriamali mbali mbali wa huduma na bidhaa za utalii. Kukamilka kwa mafunzo hayo kumepelekea kuwawezesha wamiliki wa mahoteli kutoa huduma bora ambazo zinaendana na soko la kimataifa la utalii.

## SEKTA YA MAMBO YA KALE

### i. Kuimarika kwa uwekezaji katika maeneo ya kihistoria na Mambo ya Kale.

Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo hususan Oman, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Big Z, na Kampuni ya Infinity Cultural Development na Heritage Foundation katika kuyaokoa, kuyakarabati, na kuyaendeleza majengo na maeneo muhimu ya kihistoria ndani ya Mji Mkongwe na sehemu nyengine. Kuimarishwa kwa maeneo hayo kunapelekea kuongeza idadi ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini pamoja na kuendelea kuuhifadhi Mji Mkongwe wa Zanzibar katika urithi wa dunia kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae.

ii. **Kuwapatia maafisa elimu ya kukusanya taarifa za maeneo ya kihistoria na urithi wa Mambo ya Kale kwa njia za kidijitali**

Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha St. Andrews cha Scotland, Royal Agricultural Univeristy, American University of Sharjah imeendeela kuimarisha elimu, utafiti, upimaji , ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa kuhusiana na uchimbaji wa kiakiolojia, utunzaji na uhifadhi wa urithi wa mambo ya kale na vitu vya kihistoria ikiwemo matumizi ya njia za kidijitali. Mashirikiano haya yameiwezesha Wizara kuwa na wataalamu zaidi wenye taaluma bora na ya kisasa ya kuweza kutunza na kuhifadhi mambo ya kale na kutunza kumbukumbu hizo kwa muda mrefu sana na kubaki katika katika hali yake ya asili.

iii. **Kuwapatia maafisa mafunzo ya uendeshaji wa mfumo wa kanzi data "data base" na Majengo ya Kale na maeneo ya Kiakiolojia**

Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha York cha nchini Uingereza kupitia mradi wa Mapping Africa's Endangered Archaeological Sites and Monuments (MAESAM), kiliwapatia mafunzo ya kutengeneza na kuingiza taarifa za mfumo wa kidijitali za majengo ya kale na maeneo ya kiakiolojia ambayo yapo hatarini kutoweka. Mafunzo hayo yalifanywa kwa maafisa wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Mafunzo hayo yanasaidia kutunza taarifa, kuhifadhi na kuweka kumbukumbu za majengo ya kale na maeneo ya kiakiolojia ambayo yapo hatarini kutoweka.

Vile vile Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Oman imeendelea na mchakato wa ukarabati wa majengo ya Peace Memorial, Beit el Ajaib, Jumba la Wananchi (People's Palace), Beit Oman, Beit Barghash, Grand Palace, Kibweni Palace, na Beit Mtoni. Halikadhalika, kupitia Kampuni ya Infinity Cultural Development, Wizara inashirikiana na kampuni hii katika mfumo wa PPP katika kukarabati na kuyaendeleza majengo ya Mahakama Kuu ya Vuga, Ngome Kongwe, Jengo la kihistoria la Karavan Serai lililopo Hurumzi, Bustani za Mji Mkongwe, Mahamam ya Hamamni, Forodhani, Kidichi, na Kizimbani. Pia Kampuni hii imesaidia sana kuwawezesha wajasiriamali wa bidhaa za kitalii kuweza kufanya biashara zao katika maeneo mazuri ambayo yatawavutiwa wageni na kuongeza haiba ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

**v. Kuyapatia Hati miliki maeneo ya Kihistoria**

Katika kuyatunza, kuyaendeleza na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria yasipotee na kuvamiwa, Wizara imeendelea kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi katika kuyapatia hati miliki maeneo yote ya kihistoria na yenye umuhimu wa kipekee katika historia ya Zanzibar. Wizara hadi sasa imefanikiwa kuyapatia Hati Miliki maeneo 31 ya kihistoria Unguja na Pemba miongoni mwa maeneo yaliyotangazwa kisheria. Miongoni mwao ni jengo la Beit el Ajaib, Ngome Kongwe, eneo la kihistoria la Pango la Mangapwani na eneo la kihistoria Jumba la Wananchi Forodhani.

## E. CHANGAMOTO ZA WIZARA NA UTATUZI WAKE

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale licha ya kufanikiwa pia inakabiliwa na Changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

| NA | CHANGAMOTO | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| i. | Ushiriki mdogo wa taasisi za Serikali katika kuitangaza Zanzibar katika masoko ya kimataifa. | Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi za ndani na nje ya nchi zimefanikiwa kuyafikia masoko zaidi ya kimataifa ya hadhi ya juu ili kuweza kupata idadi kubwa ya watalii na mapato zaidi. |
| ii. | Ushindani wa biashara ya utalii kutoka nchi zenye huduma na bidhaa zinazofanana na Zanzibar. | Wizara inaendelea na hatua za kuimarisha ubora wa huduma na bidhaa kwa wageni wanaoingia nchini ili waweze kuvutiwa zaidi na pia katika juhudi za kulifungua zaidi Soko la Watalii Kutoka Barani Afrika na Asia. |
| iii. | Uvamizi wa biashara zinazotakiwa kufanywa na wazawa na badala yake kuchukuliwa na wageni kinyume na Sheria ya Utalii. | Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii imeimarisha mikakati ya kukabiliana na biashara haramu zinazofanywa na wageni kinyume na Sheria ya Utalii ya Zanzibar. |

| NA | CHANGAMOTO | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| iv. | Uhaba wa rasilmali fedha katika kuimarisha mifumo ya ugavi na mnyororo wa thamani wa sekta ya utalii katika kufanikisha dhana ya Utalii kwa Wote inayowagusa wananchi wa kawaida. | Mbali na Serikali kuwekeza sana katika uwezeshaji wa ajira kwa vijana kupitia mikopo isiyo na riba, kuwapatia nyenzo na mbinu za ujasiriamali wa kisasa pamoja na kuwatafutia masoko ya bidhaa zao za kitalii, Wizara pia imekuwa ikishirikiana na wadau wa maendeleo kama Benki ya Dunia (BIG Z Project), Umoja wa Ulaya (Blue Economy for Climate Resilience and Job Creation) na miradi ya maendeleo ya SMZ katika kupanua wigo wa elimu na uwezeshaji kwa vijana katika ujasiriamali wa sekta ya utalii. |
| v. | Matumizi haba ya mifumo ya kidijitali na AI katika kuitangaza, kuipima na kuiendeleza sekta ya utalii. | Wizara imekuwa ikishirikiana na UNDP Chuo cha IIT-M na Sekta binafsi katika utengenezaji na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kuitangaza Zanzibar kiutalii lakini pia katika kuboresha mifumo yake ya huduma na mawasiliano. |
| vi. | Uchakavu wa majengo ya Mji Mkongwe na miundombinu. | Wizara imeanza kutekeleza mradi maalumu wa ukarabati wa nyumba hatarishi ndani ya Mji Mkongwe ambao lengo la mradi huu ni kurudisha haiba na hadhi ya nyumba zilizopo ndani ya Mji Mkongwe. Hadi sasa majengo manne yamekarabatiwa na kukamilika. |

| NA | CHANGAMOTO | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| vii. | Uvamizi wa maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini. | Wizara inaendelea kuchukua hatua za makusudi za kuyapima na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria pamoja na kuyapatia hati miliki ambapo kwa sasa maeneo 31 yameshapatiwa hatimiliki kwa Unguja na Pemba. |
| viii. | Ukiukwaji wa masharti ya vibali kwa mujibu wa nyumba za Mji Mkongwe ambao huyafanyia matengenezo majengo yao kinyume na vibali walivyoomba | Wizara inaendelea na jitihada za kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ukarabati unafanyika kwa mujibu wa vibali vinavyotolewa pamoja na kuwaelimisha wakaazi na wadau wa Mji Mkongwe. Aidha, wanaokiuka masharti ya vibali hutozwa faini kwa mujibu wa sheria ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. |

## F.FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025-MACHI 2026)

**13. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale iliidhinishiwa fedha za matumizi na Baraza la Wawakilishi **Shilingi 45,032,022,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo **Shilingi 3,210,300,000/=** zilikuwa ni kwa kazi za kawaida, **Shilingi 4,795,900,000/=** zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara. Kati ya hizo **Shilingi 3,646,500,000/=** zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya taasisi zisizopokea

ruzuku na **Shilingi 1,149,400,000/=** zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya taasisi zinazopokea ruzuku.

Vile vile, **Shilingi 37,025,822,000/=** zilikuwa ni kwa kazi za Maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 22,000,000,000/=** ni fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na **Shilingi 15,025,822,000/=** ni fedha kutoka Serikali ya Oman kwa ajili ya matengenezo ya jengo la Beit el Ajaib. Pia, Wizara iliidhinishiwa makusanyo ya mapato ya **Shilingi 2,250,000,000/=** zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Aidha, Kamisheni ya Utalii iliidhinishiwa makusanyo ya matumizi ya **Shilingi, 11,668,715,869/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu mbili. Kati ya hizo **Shilingi 2,582,899,269/=** zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 7,085,816,600/=** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na **Shilingi 2,000,000,000/=** zilikuwa ni fedha zilizopangwa kuingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina.

Pia, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe iliruhusiwa kukusanya na kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vyake vya mapato ambayo jumla yake ilikuwa ni **Shilingi, 3,600,000,000/=** kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji na utoaji huduma.

**14.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2026, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilipokea jumla ya **Shilingi 17,185,686,438.27/=** sawa na asilimia 38.16. Kati ya fedha hizo **Shilingi 852,529,931.7/=** zilipatikana kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia **26.56. Shilingi 3,396,707,904.50/=** zilipatikana kwa ajili

ya mishahara sawa na asilimia **70.83.** Aidha, **Shilingi 12,936,448,602.07** zilipatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sawa na aslimia **34.94** na kati ya hizo **Shilingi 406,013,683/=** zilipatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo ni sawa na asilimia 1.84, na **Shilingi 12,530,434,919.07/=** zilipatikana kwa ajili ya utekelezaji wa mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Oman ambayo ni sawa na asilimia **83.39.**

Aidha, Kamisheni ya Utalii ilifanikiwa kupata **Shilingi 1,789,745,170/=** kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 69.20 na **Shilingi 5,041,757,945/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 71.1.

Pia, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ilifanikiwa kupata **Shilingi 2,287,677,102/=** kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji na utoaji huduma ambayo ni sawa na asilimia **63.50**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1A na 1C).**

## G. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

**15. Mheshimiwa Spika,**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza Malengo na Majukumu kwa kufuata mfumo maalumu wa bajeti (Program Based Budget, PBB), ambapo Wizara inasimamia programu kuu tano na programu ndogo tatu.

**Programu Kuu za Wizara ni : -**

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
ii. Programu ya kusimamia Maendeleo ya Utalii.
iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.
iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.
v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

**Programu ndogo za Wizara ni: -**

i. Kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.
ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale.
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

## H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**16. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilipanga kutekeleza Programu ya Kuimarisha na kuendeleza Maeneo ya kihistoria kwa kuyafanyia matengenezo maeneo yafuatayo:-

i. Kuweka uzio katika maeneo ya kihistoria
ii. Kuanzisha na kutengeneza Makumbusho ya Biashara
iii. Kuanzisha na kutengeneza Makumbusho ya sanaa
iv. Kuanzisha na kujenga Makumbusho ya Mwera
v. Kutengeneza Makumbusho ya Amani na Viumbe hai pamoja na Bustani ya Victoria

vi. Ukarabati wa Majengo Hatarishi ndani ya Eneo la Mji Mkongwe
vii. Mradi wa kuimarisha Vivutio vya Utalii Zanzibar

**17. Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kukuarifu kwamba katika mwaka wa fedha 2025/2026, miradi hii ipo katika hatua za manunuzi. Aidha, Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi ambayo fedha zake ziliidhinishwa katika bajeti za nyuma na ambayo utekelezaji wake haukukamilika kwa mujibu wa wakati uliopangwa kutokana na changamoto mbali mbali za taratibu za uidhinishaji wa kifedha, kiutekelezaji na uchelewaji wa malighafi kutoka nje ya nchi. Miradi hiyo ni kama ifuatvyo:-

**Mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba.**

**Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu-Pemba**

Mradi wa Kuimarisha eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba unatekelezwa na kampuni ya Yassin & Sons Limited. Mradi huu umepangiwa jumla ya **Shilingi 2,407,316,675/=** hadi kukamilika kwake. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi Wizara imefanya malipo ya **Shilingi 383,534,213/=**. Fedha zote ambazo amelipwa Mkandarasi hadi sasa ni **Shilingi 1,371,405,785.5** sawa na asilimia **57** ya bajeti ya Mradi wote. Utekelezaji uliobakia wa mradi huu kwa kipindi hichi ni utengenezaji wa njia ndogo ya kuingia katika eneo la kihistoria, uimarishaji wa bustani (landscaping), uwekaji alama za mipaka ya eneo la kihistoria, pamoja na ujazo wa kifusi nyuma ya ukuta wa kuzuia maji. Hadi sasa utekelezaji umefikia asilimia **95**.

**Eneo la Kihistoria la Mangapwani - Unguja**

Mradi wa kuimarisha eneo la Kihistoria la Mangapwani Unguja unatekelezwa na Kampuni ya Al Hilal Company LTD. Mradi huu umegharimu **Shilingi 2,238,544,230/=** na hadi kufikia Machi 2026 mjenzi amelipwa **Shilingi 1,948,706,869.43/=** sawa na asilimia **87** ya malipo na utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia **95.** Mradi huu unahusisha ukarabati wa maeneo makuu matatu ya kihistoria ambayo ni Kisima cha Chini kwa Chini, Mabaki ya Mahandaki ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia pamoja na Chemba au Handaki la Kuhifadhia Watumwa. Hadi sasa kazi zilizofanyika katika maeneo haya ni pamoja na ujenzi wa majengo mapya ya maduka, ofisi na mkahawa, Ukarabati wa ngazi za kushukia katika Kisima cha Chini kwa Chini, Ukarabati wa Mahandaki ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, Ukarabati wa Handaki lililotumika Kuhifadhia Watumwa, kuchimba kisima, kuweka vigae vya njiani, kuchimba kisima na kusambaza maji katika maeneo yote, kuweka huduma za umeme pamoja na ujenzi wa ukuta kwa ajili ya kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria yaliyopo katika eneo hilo. Kazi zilizobaki hivi sasa ni hatua ya kusaili ukamilishaji "Snags & Quality Control Process" kabla ya mchakato wa hatua na makabidhiano kuanza baadaye mwaka huu. Aidha,Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imefanya malipo ya **Shilingi 22,479,470/=** kwa Mkandarasi Modern Building Contractor kwa ajili ya malipo baada ya kumaliza ujenzi (Retention) wa jengo la ofisi lililomo ndani ya Wizara. Kukamilika kwa jengo hilo kumepelekea kupunguza changamoto ya uhaba wa ofisi kwa wafanyakazi.

**Mradi wa Ukarabati wa Nyumba Hatarishi za Mji Mkongwe**

**18. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe inaendelea kutekeleza, kuimarisha na kuuendeleza Mji Mkongwe kwa kuyafanyia matengenezo makubwa majengo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe ili uendelee kubakia kuwa urithi wa Kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilipangiwa Shilingi **10,000,000,000/=** kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati nyumba 10 zilizopo ndani ya Mji Mkongwe na hadi kufikia Machi 2026 mradi huu bado haujaingiziwa fedha za malipo kwa mkandarasi, ingawa utekelezaji wa mradi huu kwa baadhi ya maeneo ukiendelea kupitia mfuko maalum wa hifadhi ya Mji Mkongwe. Wizara imeyafanyia matengenezo makubwa majengo matano ambapo kwa sasa majengo mawili yamekamilika na majengo manne yapo katika hatua za mwisho na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

**Jengo namba 2312 (Jengo la Culture) –Vuga**

**19. Mheshimiwa Spika,** Ukarabati wa Jengo namba 2312 –Vuga. Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya K'S Builders Ltd na umegharimu Shilingi 480,470,075.60/= na Mkandarasi amelipwa Shilingi 480,470,075.60/= sawa na asilimia 100. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kurekebisha paa, dari, vyoo, kuweka plasta, kupaka rangi, kufanya "fitting" ya umeme na maji, ufungaji wa milango na madirisha pamoja na uwekaji wa sakafu. Utekelezaji wake umeanza Novemba 2024 na ulikamilika Julai 2025. Utekelezaji wa Mradi huu umefikia asilimia 100 na tayari

jengo limekabidhiwa kwa wamiliki wake ambao ni "Culture Music Club".

**Jengo namba 1196/97 - Malindi**

**20. Mheshimiwa Spika,** Ukarabati wa Jengo namba 1196/97 - Malindi. Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya M/s Yassin & Sons Company Ltd na unagharimu **Shilingi 472,158,100/=** na hadi kufikia Machi, 2026, Mkandarasi amelipwa **Shilingi 240,000,000/=** sawa na asilimia **50.8** ambapo kazi zilizofanyika ni ujenzi wa paa, ujenzi wa dari, boriti, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka mifumo ya umeme, maji safi na maji taka pamoja na upakaji rangi. Fedha hizi zinatoka katika Mfuko wa Hifadhi ya Mji Mkongwe. Aidha, kwa sasa Mkandarasi anamalizia sehemu ambazo alitakiwa kufanya marekebisho ili aweze kukabidhi mradi. Utekelezaji wake umeanza Disemba 2024 na unatarajiwa kukamilika Aprili, 2026. Mradi huu umefikia asilimia **95**.

**Jengo namba 1065- Malindi Funguni**

**21. Mheshimiwa Spika,** Ukarabati wa Jengo namba 1065-Malindi Funguni. Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya Kin Investment Company Ltd na umegharimu **Shilingi 742,862,222.5/=** na Mkandarasi amelipwa **Shilingi 742,862,222.5/=** sawa na asilimia **100**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa paa, ujenzi wa dari na boriti, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka mifumo mipya ya umeme, maji safi na maji taka pamoja na upakaji rangi. Utekelezaji wake umeanza Novemba 2024 na umekamilika Novemba, 2025.

**Jengo namba F06A- Forodhani**

**22. Mheshimiwa Spika,** Ukarabati wa Jengo namba F06A-Forodhani. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Faster Company Limited. Mradi huu unagharimu **Shilingi 713,680,512.50/=** hadi kufikia Machi 2026, Mkandarasi amelipwa **Shilingi 248,195,297/=** sawa na asilimia **34.8.** Fedha hizi zinatoka katika Mfuko wa Hifadhi ya Mji Mkongwe. Kazi zilizofanyika ni ukarabati wa paa, kukamilika kwa ujenzi wa ghorofa ya pili na ghorofa ya kwanza, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka mifumo mipya ya umeme, maji safi na maji taka kwa ghorofa ya kwanza na ghorofa ya pili. Utekelezaji wake umeanza kutekelezwa Januari 2025 na unatarajiwa kukamilika Aprili 2026. Mradi huu umefikia asilimia **75**.

**Jengo namba 719- Malindi.**

**23. Mheshimiwa Spika,** Ukarabati wa Jengo namba 719-Malindi. Mradi huu unatekelezwa na K'S Builders Limited. Mradi huu unagharimu **Shilingi 394,494,277.88/=**. Hadi kufikia Machi 2026, jengo limekabidhiwa kwa Mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi na kazi zinazotarajiwa kufanyika ni ukarabati wa paa, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka sakafu, kubadilisha boriti mbovu na kuweka mpya na kuweka mifumo mipya ya umeme, maji safi na maji taka. Utekelezaji wake umeanza Machi 2026 na unatarajiwa kukamilika Novemba 2026.

**Mradi wa Ukarabati wa Beit Al Ajaib**

**24. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ufadhili wa Serikali ya Oman, inaendelea kushirikiana na wakandarasi wa Mradi huo kwa kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu wa pamoja katika kazi za Ukarabati wa mradi wa Jengo la Beit-el –Ajaib. Mkandarasi wa mradi ni "Nandhra Engineering & Construction Company" na Mshauri elekezi wa mradi huu ni "Distruct Solution" kutoka Lebanon. Utekelezaji wa Mradi huu umeanza Machi 2023 na unatarajiwa kukamilika Disemba 2026. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Oman na unagharimu Dola za Kimarekani Milioni 21 ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 **Shilingi 15,025,822,000/=** zilitengwa na hadi kufikia Machi 2026 Mkandarasi amelipwa **Shilingi 12,530,434,919.07/=** sawa na asilimia 83.39. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uimarishaji wa msingi wa jengo, ukarabati wa nguzo za jengo, uokozi na ukarabati wa milango ikiwemo Mlango mkubwa wa mbele, madirisha na samani zilizoathirika wakati wa ajali ya jengo hilo, ujenzi wa upande wa ukuta ulioanguka, kazi za maji na umeme, kazi za kuweka veranda na balcony na kuanza kuweka dari ya zege sehemu ya juu iliyovunjika.

**25. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuzifanyia matengenezo nyumba nyengine za Mji Mkongwe kwa lengo la kuweza kuubakisha Mji huo na kuendelea kuwa miongoni mwa urithi wa dunia ambao unapelekea kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini.

## I. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2025-MACHI 2026

**26. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilipanga kutekeleza programu kuu tano kama ifuatavyo:-

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
ii. Programu ya kusimamia Maendeleo ya Utalii.
iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.
iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.
v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

## I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

**27. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuhakikisha uhifadhi wa matumizi endelevu ya eneo la urithi la Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa, kuimarishwa na kutunzwa kwa faida ya vizazi vya sasa na vya baadae. Matokeo ya muda mrefu ni kuyahifadhi, kuyalinda, kuyatangaza na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na kuuhifadhi Mji Mkongwe ili ubaki kuwa urithi wa kimataifa.

**28. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe

**29. Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa na programu hii ni Uhifadhi na uendelezaji wa Makumbusho, Maeneo ya Kihistoria, Mambo ya Kale pamoja na Mji Mkongwe.

**UTEKELEZAJI HALISI**

**30. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho ilifanikiwa kuvitangaza vivutio na maeneno ya kihistoria kikanda, kitaifa na kimataifa kwa kufanya vipindi pamoja na kushiriki katika maonesho ya biashara ya miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari lilofanyika Gana Unguja na ilishiriki katika kongamano la wadau wa Utalii na Mambo ya Kale kisiwani Pemba. Aidha Idara ilirusha hewani vipindi 18 vya Radio na TV ikiwemo vipindi 10 Tanzania safari Channel TV, vipindi vinne vya ZBC Radio, vipindi viwili TBC TV, Alfalaah TV kimoja, na Kipindi kimoja ZBC TV. Hii ilikuwa ni kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya kihistoria na Maeneo ya Kale. Pia, jumla ya wageni 36,412 wametembelea maeneno ya kihistoria kwa Unguja na Pemba, kati ya hao wageni wa ndani ni 2,046 wakati wageni wa nje 34,366.

**31. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale inaendelea na jitihada zake za kuyapatia Hatimiliki maeneo mbali mbali ya kihistoria yaliyopo nchini kwa lengo la kuyatunza, kuyaendeleza na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria ili yasivamiwe. Hadi kufikia mwaka 2025/2026, Idara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi tayari imeshafanikiwa kuyapatia hatimiliki jumla ya maeneo 31 kati ya maeneo yote yaliyotangazwa kwa mujibu wa Sheria.

32. **Mheshimiwa Spika, katika** kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa jamii, Idara iligharamia masomo ya wafanyakazi watatu wa muda mrefu. Mmoja ngazi ya shahada ya kwanza ya Recording Management and Archives katika Chuo cha Utawala wa Umma (IPA), mmoja fani ya Human Resource and Management katika Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na mmoja ngazi ya Astashahada ya Heritage Management katika Chuo cha Utalii Maruhubi. Aidha, Idara ilifanya mafunzo ya kupima na kukusanya taarifa za Maeneo ya Urithi wa Mambo ya Kale ambayo yapo hatarini kutoweka kwa njia ya Kidijitali. Pia, Idara ilitoa mafunzo mafupi kwa mfanyakazi mmoja kwenda Sharjah Institute of Heritage kujifunza mafunzo ya "Conservation of Heritage Buildings". Halikadhalika, Idara kwa mashirikiano na Makumbusho ya Taifa ya Oman iliendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake wawili kupata taaluma ya uhifadhi wa vitu tofauti vya Makumbusho kama vile mbao, nguo, karatasi na Mazulia kwa mtindo wa kinadharia na kivitendo nchini Oman.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika kuyatunza na kuyasimamia Maeneo ya kihistoria na Mambo ya Kale, Idara ilifanya malipo kwa walinzi wa JKU, walinzi wa Mkataba na walinzi wa ndani kwa Unguja na Pemba. Pia ililipa stahiki mbali mbali za wafanyakazi zikiwemo likizo, ufiwa, masaa baada ya kazi, chakula cha wanyama na huduma za ofisi.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Mji unakwenda sambamba kwa mujibu wa Sheria nambari 4 ya Mji Mkongwe ya mwaka 2010, na Sheria nambari 6 ya mwaka

2023 pamoja na Mkataba wa Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO convention 1972), Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe inaendelea kudhibiti ujenzi, biashara holela pamoja na uingiaji na uegeshaji wa vyombo vya moto usiofuata Sheria. Jumla ya vyombo vya moto vilivyovunja Sheria na kuchukuliwa hatua ni 2,118, biashara holela 519 na kuzuia ujenzi holela wa majengo matano na eneo la wazi moja. Mamlaka imechukua hatua ya kuboresha mazingira ya wajasiriamali kwa kuwapa nafasi ya kutangaza na kuuza biashara zao katika mabanda ya maonesho ambayo hufanyika kila mwezi kwa siku saba katika eneo la Forodhani. Aidha, katika kupunguza biashara holela ndani ya eneo la Hifadhi, Mamlaka imeanza kuwapanga wafanyabiashara katika eneo la Jumba la Treni, Darajani na Kinazini.

**35. Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuweka muonekano mzuri na wenye kuvutia katika maeneo ya Mji Mkongwe, Mamlaka imepokea maombi 136 ya vibali vya ujenzi, vibali 127 vimetolewa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na vibali tisa kwa ajili ya ujenzi mpya. Mamlaka inaendelea kurejesha haiba ya maeneo mbali mbali ya Mji Mkongwe kwa kuweka sawa njia za watembea kwa miguu, kuweka vigae (pavements) katika njia, kurejesha haiba ya Bustani zilizomo Mji Mkongwe kwa kupanda miti ya maua, kuweka taa katika miti yote inayozunguka uwanja wa Mnazi Mmoja na Bustani ya Tenga pamoja na kubadilisha bomba ya maji taka na kuweka mpya katika eneo la Mbuyuni hadi Darajani, kuondoa mifuniko ya karo iliyoharibika na kuweka mipya.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika suala la utoaji elimu kwa wananchi na kuhakikisha kwamba wanapata elimu ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Mamlaka inaendelea kutoa elimu kupitia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo Asam TV online, ZBC TV, TBC, Zanzibar Cable TV na Bahari FM pamoja na kufanya mikutano ya makundi mbali mbali wakiwemo viongozi wakuu wa Serikali, wafanyabiashara, madereva wa vyombo vya moto, wanafunzi na Masheha wa Mji Mkongwe. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wa Mji Mkongwe imefanya maadhimisho ya siku ya Mji Mkongwe tarehe 02/12/2025. Maadhimisho haya hufanyika kila ifikapo tarehe 02 Disemba ya kila mwaka. Kauli Mbiu ya mwaka jana ilikuwa "Tukienzi Karne ya Historia, Mji Mkongwe na Baitil-Amaan, Hazina Isiyoshikika". Maadhimisho hayo hufanyika kwa lengo la kutambua thamani ya Kipekee ya Mji Mkongwe Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuelimisha jamii juu ya Mkataba wa Urithi wa Dunia pamoja na ushiriki wa Wadau katika kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya Urithi wa Dunia.

37. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi watano, mmoja alipatiwa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Maafisa kumbukumbu yaliyofanyika Dar- es- Salaam na wanne mafunzo ya kujenga uwezo kwa wataalamu wa Urithi wa Miji ya Urithi wa Dunia yaliyofanyika Sharjah,UAE.

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imehudhuria vikao viwili vya 43 na 47 vya UNESCO vilivyojumuisha nchi wanachama wa UNESCO. Kimoja kilichofanyika nchini Ufaransa na na chengine kilichofanyika nchini Uzbekistan vikao hivi vilikuwa na lengo la kujadili hali ya uhifadhi ya kila kituo cha urithi wa Dunia na kutolea maamuzi ya kuendelea au kutoendelea kuwepo katika orodha ya Miji ya Urithi wa Dunia. Vikao hivi hufanyika kila mwaka ili kujadili mwenendo wa Uhifadhi katika kila nchi Mwanachama wa UNESCO. Vilevile, Mamlaka imehudhuria Tamasha la siku ya Urithi wa Sharjah (Sharjah Heritage Day) lililofanyika Sharjah katika Mji wa Sharjah Old Town likiwa na lengo la kutambua thamani ya Mji huo pamoja na kujifunza kuhusiana na umuhimu wa kuthamini Miji ya Urithi wa Dunia ili iendelee kuwepo kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Aidha, Mamlaka imeshiriki kikao cha kuandaa Mpango Mkakati wa ushiriki wa Tanzania kwenye Kamati ya Urithi wa Dunia kwa kipindi cha mwaka 2025-2029 na kikao cha kujadili ripoti ya hali ya uhifadhi wa Miji ya Urithi wa Dunia kilichofanyika Dar-es-Salaam.

**39.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 34,158,246,575/=**. Hadi kufikia Machi 2026 progarmu hii imefanikiwa kupata **Shilingi 14,846,012,416.55/=** sawa na asilimia **43.46. Shilingi 520,370,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na hadi kufika Machi 2026 **Shilingi 124,012,115.98/=** zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia **23.83**. Vile vile **Shilingi 2,612,054,575/=** ziliidhinishwa kwa ajili

ya mishahara, na hadi kufikia Machi 2026 programu hii imefanikiwa kupata **Shilingi 1,785,551,698.85/=** sawa na asilimia **68.36** ya makadirio.

Programu hii pia ilipangiwa **Shilingi 31,025,822,000/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kati ya hizo **Shilingi 16,000,000,000/=** ni fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2026 imepata **Shilingi 406,013,683/=** sawa naasilimia **1.84.** na **Shilingi 15,025,822,000/=** ni fedha kutoka Serikali ya Oman na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 12,530,434,919.07/=** sawa na asilimia **83.39**. Aidha, Programu hii ilitakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 2,240,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2026 imekusanya jumla ya **Shilingi 1,269,323,873/=** sawa na asilimia **56.67 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1B, 1C na 1D).**

Pia, Programu hii ilitakiwa kukusanya na kutumia **Shilingi 3,600,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2026 imekusanya na kutumia jumla ya **Shilingi 2,287,677,102/=** sawa na asilimia **63.50 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1B na 1D).**

### II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya utalii nchini. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya nchi na wananchi. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utalii.

## UTEKELEZAJI HALISI

40. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanikiwa kuibua vivutio vipya vya utalii vitano Unguja na Pemba ikiwemo kijiji cha Muungoni na Uzi kwa Unguja na kwa upande wa Pemba ni eneo la Pango Samaki, Kisiwa Ndege na Mtofuraha. Aidha, Idara iliweza kufanya ukaguzi katika maeneo ya vivutio vya utalii 13 na operesheni nane Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za utalii pamoja na kukagua huduma za kitalii zinazotolewa na kuona namna gani Sera ya Utalii inatekelezwa kwa kuendeleza maeneo ya vivutio vya utalii katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba

41. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuwa na mpango endelevu wa ushirikishwaji jamii katika mnyororo wa thamani katika utalii, Idara imeandaa mpango mkakati wa miaka mitano wa "Community-Based Tourism" wenye lengo la kuishirikisha jamii moja kwa moja katika shughuli za utalii na kuwapatia elimu ya kuibua fursa za utalii zilizokuwepo katika maeneo wanayoishi sambamba na dhana ya Utalii kwa Wote.

42. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanikiwa kuratibu na kukamilisha ugatuzi na usajili wa Chuo Cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar (ZIToD). Kwa sasa Chuo hicho kimesajiliwa na kupatiwa ithibati na Baraza la Elimu la Ufundi Stadi na Mafunzo ya Amali Tanzania (NACTIVET). Hapo awali Chuo hiki kilikuwa chini ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Vile vile, Wizara ipo katika mikakati ya kukiimarisha Chuo hicho na kuhakikisha kinatoa wahitimu

watakao kuwa na uwezo wa kutoa huduma za hoteli, ukarimu na fani nyengine za kiutalii katika masoko na ajira za ndani na nje ya nchi kwa mashirikiano na taasisi za elimu za kimataifa zenye vyeti vinavyotoa ithibati yenye kutambuliwa kimataifa.

**43. Mheshimiwa Spika,** Idara imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa fani ya utalii ndani ya nchi kwa mfanyakazi mmoja katika kiwango cha Shahada ya kwanza na wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya utalii nje ya nchi katika kiwango cha Shahada ya Uzamili. Pia, Idara imewapatia mafunzo ya ndani ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi 22, na wafanyakazi wawili walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya utalii nchini India na China. Vile vile katika kuimarisha ufuatiliaji wa kazi Idara imenunua pikipiki nne kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za Idara kwa Maofisa utalii wa Wilaya na Makao Makuu.

**44. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha jitihada za kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi, Idara imefanikiwa kurusha hewani jumla ya vipindi tisa kupitia vyombo vya habari mbali mbali vilivyopo nchini ikiwemo ZBC TV, ZBC Redio, Bahari FM Redio, Pemba Today Online, BM Swahili online na pia Makala moja iliyochapishwa kupitia Gazeti la Zanzibar Leo inayohusu utalii pamoja na kukutana na wadau wa utalii kwa ajili ya kujadili njia bora za kuendeleza utalii Unguja na Pemba. Aidha, Idara imefanikiwa kuingia makubaliano na kampuni ya Zanzibar Cable Television ya kuanzisha chaneli ya utalii na kuwezesha kurushwa hewani Chaneli hiyo kupitia kisimbuzi cha Zanzibar

Cable Television. Pia, Idara inaendelea na mazungumzo ya mwisho na Kampuni ya AZAM Media ili chaneli hiyo kuweza kupatikana kupitia kisimbuzi cha AZAM ambapo itapatikana dunia nzima. Hizi ni katika jitihada za Wizara za kuutangaza utalii na kutoa uelewa ndani na nje ya nchi.

45. **Mheshimiwa Spika,** Ili kufanikisha utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote, Idara imeratibu utendaji wa Kamati za Utalii za Wilaya pamoja na wananchi Unguja na Pemba, ambapo ufuatiliaji wa ushiriki wa makundi mbalimbali katika shughuli za utalii umefanyika na ilifanikisha ziara ya watu wenye mahitaji maalumu 100 wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kusini Pemba waliotembelea vivutio vya utalii vya Unguja, ili kuhakikisha uhamasishaji wa utalii wa ndani na utalii kwa wote.

46. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeshiriki katika bonanza na maonesho mbali mbali yakiwemo maonesho ya Saba Saba, maonesho ya biashara ya kitaifa Zanzibar (ZITF) maonesho ya Mapinduzi na Kili Fair Arusha, Zanzibar Tourism Summit pamoja na Bonanza la Utalii Pemba (Tourist Sport Bonanza kwa lengo la kuwafikia wadau wa utalii kwa kuelimisha, kusikiliza na kupokea maoni pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma na kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya utalii.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza utalii wa michezo, Idara imeratibu ziara ya mwanamasumbwi wa kimataifa wa mchezo wa masumbwi kutoka Ujerumani aitwaye Maximilian Herman Hans maarufu kama ‘Max Coga, ambaye pia alitembelea kisiwani Pemba na kufanya

maonesho Gombani na kisiwa kidogo cha Kojani pamoja na kuratibu matembezi ya mabalozi na wageni mashuhuri waliofika Zanzibar na kupata fursa ya kutembelea katika vivutio vya utalii.

48. **Mheshimiwa Spika,** Ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa masoko katika sekta ya utalii kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati, Idara imewakutanisha wajasiriamali wa bidhaa za utalii wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini Unguja, Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkoa wa Kusini Pemba pamoja na wafanyabiashara wa huduma za kitalii wakiwemo wenye mahoteli kama njia ya kuwapatia masoko ya bidhaa zao na kuongeza matumizi ya bidhaa za utalii nchiniyaani 'local content' katika soko la utalii. Jitihada hii imelenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kitalii kwa wafanyabiashara wadogo wadogo.

49. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeratibu mafunzo ya utalii endelevu kwa wadau wa utalii Unguja na Pemba yaliyofadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) na mengine yaliyofadhiliwa na kuendeshwa na Chuo Kikuu cha Royal Agricultural University cha Uingereza kwa maofisa utalii, waandaaji misafara ya kitalii, wanaotoa huduma za kitalii zikiwemo hoteli na waongoza watalii, wajasiriamali wa bidhaa za utalii na waendesha mashamba ya viungo kwa watalii, kwa lengo la kuwawezesha kutoa huduma katika sekta ya Utalii kulingana na viwango vya soko la Utalii Duniani ili kuendeleza dhana ya utalii endelevu.

50. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeratibu mikutano ya wadau iliyozungumzia namna bora ya kuendesha utalii kwa kizingatia dhana ya utalii endelevu pamoja na mikakati ya harakati za maendeleo ya utalii wenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira kwa kuwashirikisha wadau wa sekta binafsi na sekta za umma kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika kutatua changamoto zilizopo pamoja na kuwashirikisha wadau katika mipango ya maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

51. **Mheshimiwa** Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 6,984,181,546/=** na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 331,864,310.95/=** sawa na asilimia **4.75**. **Shilingi 694,210,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufika Machi 2026 **Shilingi 127,446,710.95/=** zilipatikana sawa na asilimia **18.36**. Vile vile, **Shilingi 289,971,546/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara, na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 204,417,600/=** sawa na asilimia **70.50** ya makadirio. Program hii pia ilipangiwa **Shilingi 6,000,000,000/=** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, na hadi kufikia Machi 2026 programu hii haijafanikiwa kupata fedha za miradi hiyo. **(tafadhali angalia kiambatanisho namba 1C na 1D).**

## III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

52. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni kituo bora cha utalii duniani. Pia kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

## UTEKELEZAJI HALISI

53. **Mheshimiwa Spika,** ili kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi Kamisheni ya utalii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa utalii kutoka Zanzibar na Tanzania Bara imeshiriki maonesho ya utalii ya kimataifa ya "IFTM Topresa Exhibition" yaliyofanyika nchini Ufaransa, maonesho ya "FITUR Exhibition" yaliyofanyika mjini Madrid - Hispania pamoja na maonesho ya "World Travel Market" yaliyofanyika jijini London nchini Uingereza. Vile vile, katika kuhamasisha utalii wa ndani Kamisheni ya Utalii imeshiriki katika maonesho ya Kusini International Trade Fair yaliyofanyika Mkoani Mbeya, maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba) jijini Dar Es Salaam, maonesho ya Kimataifa ya Biashara (ZITF) yaliyofanyika Nyamanzi-Zanzibar, maonesho ya Halal Exhibition yaliyofanyika Zanzibar pamoja na maonesho ya Z-Summit yaliyofanyika

Zanzibar. Aidha, Kamisheni ya Utalii iliandaa Tamasha la Utalii na Utamaduni “Pemba Tourisport Bonanza and Culture” ambalo lilijumuisha michezo na shughuli mbali mbali za utalii ikiwemo mchezo wa ng’ombe, resi za ngalawa, mashindano ya dufu, paredi ya punda, ngoma za asili, ziara katika maeneo ya utalii, kuogelea, triathlon (kuogelea, kupanda baiskeli na kukimbia) na Duathlon (kukimbia na kupanda baiskeli). Lengo la kuandaa na kushiriki katika maonesho hayo ni kuitangaza Zanzibar na vivutio vyake ndani na nje ya nchi.

54. **Mheshimiwa Spika,** katika kuutangaza utalii wa Zanzibar Kamisheni iliwaalika na kupokea watu mashuhuri akiwemo Braydon Bent ambae ni mwanamtandao maarufu (influencer) anayetoka nchini Uingereza na anayeishabikia timu ya Manchester City kuja kuitembelea Zanzibar kwa lengo la kuona vivutio vya utalii vilivyopo nchini ili kuwa mabalozi wa kuitangaza Zanzibar kiutalii katika nchi zao. Aidha, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na AFRICAB imeweza kuratibu ziara ya Mrembo wa Dunia (Miss World 2025) pamoja na Mrembo wa Afrika (Miss World Africa 2025) kwa lengo la kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini na kupata fursa ya kuutangaza utalii wa Zanzibar kupitia majukwaa tofauti ya warembo hao duniani.

55. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii inaendelea na juhudi zake za kuitangaza Zanzibar Kimataifa. Katika kufanikisha azma yake hiyo, imesaini mkataba na kampuni ya SP Consulting kwa ajili ya kutangaza vivutio vya Zanzibar kwa kutumia basi linalofanya safari zake katika jiji

la London. Aidha, Kamisheni ya Utalii imesaini mkataba na kampuni ya Spark kutoka China kwa ajili ya kuhamasisha watalii kutoka China kuja kuitembelea Zanzibar pamoja na kutangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar katika majukwaa mbali mbali nchini humo.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa utalii imeendelea kuchukua hatua ya kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii waliongia hapa nchini mwaka 2025 ambapo katika mwaka huo idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia **24.5** kutoka watalii 736,755 mwaka 2024 hadi kufikia watalii **917,167** mwaka 2025.

**57.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,263,753,800 /=** kwa kazi za kawaida, na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,731,109,954/=** sawa na asilimia **137 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D)**.

## IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

**58.** **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora ya rasilimali watu katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali na mipango ya programu za kutoa huduma za utalii. Programu hii imeundwa na programu ndogo mbili ambazo ni:

i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango
ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

**59. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala kwa Kamisheni ya Utalii.

## UTEKELEZAJI HALISI

**60. Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi Kamisheni ya Utalii imehakikisha kuwa huduma mbali mbali za uendeshaji wa ofisi zinapatikana pamoja na wafanyakazi kupatiwa stahiki zao. Aidha, safari za kikazi za ndani pamoja na vikao vya mashirikiano na taasisi mbali mbali za Tanzania Bara vimefanyika.

**61. Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wake wawili wanaoendelea na mafunzo ya Shahada ya kwanza ya uwekaji kumbukumbu katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Shahada ya Uzamili katika fani ya Biashara na Uongozi katika Masoko mjini Iringa.

**62. Mheshimiwa Spika,** Kamisheni imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wake katika fani za udereva, manunuzi, uwekaji kumbukumbu na nyaraka, usalama wa mazingira kazini, mafunzo ya TEHAMA pamoja na mafunzo ya kustaafu.

**63. Mheshimiwa Spika,** katika kuwaelimisha wananchi juu ya fursa zinazopatikana katika sekta ya utalii na kuwa na

utalii endelevu unaochochea uchumi wa buluu, Kamisheni ya Utalii imeandaa na kurusha hewani vipindi mbali mbali kupitia vyombo vya habari vya Redio na Televisheni. Jumla ya vipindi 20 vimerushwa kupitia redio na televisheni za Mjini FM, Crown FM, Micheweni FM, ZBC redio na ZBC TV.

64. **Mheshimiwa Spika,** Katika kushajiisha shughuli za utalii kisiwani Pemba, Kamisheni ya Utalii Ofisi ya Pemba iliandaa ziara ya Masheha wa Shehia za Wilaya ya Chake Chake ili waweze kutambua vivutio vya utalii na historia zinazokizunguka kisiwa cha Pemba. Ziara hii ya mafunzo kwa Masheha hao ni moja ya mkakati wa Kamisheni ya Utalii katika kujenga imani kwa jamii ili kujishughulisha na huduma za utalii na kutumia fursa zilizopo ili kujiongezea kipato. Aidha, Kamisheni ya Utalii Ofisi ya Pemba, imewapatia mafunzo watoa huduma mbali mbali za utalii kwa lengo la kuwapatia mbinu na njia za kisasa za kutoa huduma za kitalii na kuvutia watalii.

65. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,631,628,800/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 2,946,984,743/=** sawa na asilimia **112.** Vile vile **Shilingi 2,582,899,269/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,789,745,170/=** sawa na asilimia **69.2** ya makadirio. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D)**.

66. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii yenye jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya utalii nchini.

**UTEKELEZAJI HALISI**

67. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeendelea kufanya ukaguzi wa miradi ya biashara za utalii ili kujiridhisha na huduma zinazotolewa pamoja na kubaini miradi inayofanya biashara kinyume na Sheria ya Utalii. Kazi hiyo imefanyika katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Katika ukaguzi huo, jumla ya miradi ya utalii 690 imekaguliwa. Miradi hiyo imejumuisha hoteli, mikahawa, michezo ya baharini na kampuni za kuandaa misafara ya watalii, ukaguzi huo uliangalia mambo mbali mbali kama vile idadi ya vyumba na wafanyakazi, huduma zinazotolewa pamoja na kutoa ushauri wa uendeshaji bora wa biashara hizo.

68. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Kampeni ya Kijani na Azimio la Utalii Endelevu (Greener Zanzibar Campaign & The Zanzibar Sustainable Tourism Declaration), Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wawekezaji katika Utalii (ZATI), iliandaa mafunzo kwa ajili ya kuhamasisha wadau wa utalii kuhusu umuhimu wa utenganishaji taka katika mahoteli. Mafunzo hayo yaliwashirikisha wadau wa utalii kama vile ZATI, ZATO, HAZ, ZATOGA pamoja na Manispaa zote za Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja.

69. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni na mali zao pamoja na sekta ya utalii kwa jumla, Kamisheni ya Utalii kupitia Kikosi cha Diplomasia na Utalii wamefanya doria maalumu 166 katika Mikoa yote mitatu ya Unguja kwa lengo la kuimarisha ulinzi na kuelimisha wananchi juu ya maeneo yanayokubalika kufanyika biashara za utalii. Miongoni mwa maeneo ambayo doria hizo zimefanyika ni pamoja na maeneo ya Mji Mkongwe, Uwanja wa Ndege, Makunduchi, Jambiani, Paje, Bwejuu, Michamvi, Kizimkazi, Pongwe, Uroa, Matemwe, Pwani Mchangani, Nungwi, Kiwengwa na Kendwa. Kufanyika kwa doria hizo kumepunguza vitendo vya uhalifu katika maeneo hayo kwa kiasi kikubwa.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 643,094,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 363,663,248/=** sawa na asilimia **57**. **(Tafadhali angalia kiambatisho nambari 1D).**

## V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

71. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale
ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

**72. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

**73. Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa katika programu ndogo hii ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi pamoja na mpango wa manunuzi.

## UTEKELEZAJI HALISI

**74. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 27 katika fani na ngazi tofauti. Aidha, wafanyakazi 15 wamepata fursa ya kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vile vile wafanyakazi 210 wamepatiwa mafunzo ya ndani juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, Mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. **(Tafadhali Angalia Kiambatanisho nambari 2).**

**75. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia ufanyaji wa tathmini ya utendaji kazi wa wafanyakazi wake wote kwa Unguja na Pemba na kujiridhisha na utendaji wao na kuwaombea nyongeza ya

mwaka. Pia, Idara imesimamia upandishaji wa madaraja kwa wafanyakazi 47. Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma na kufanya matengenezo (service) kwa vyombo vya moto ili kuhakikisha kuwa shughuli za Wizara zinatekelezwa kwa wakati na ufanisi.

76. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya ukaguzi wa ndani kwa lengo la kuhakikisha kuwa matumizi na rasilimali za Wizara zinatumika kwa mujibu wa taratibu na miongozo iliowekwa. Wizara imeendelea kufanya maboresho ya upatikanaji wa huduma za tehama kwa lengo la kuongeza ufanisi wa mawasiliano ya mtandao ndani na nje. Vile vile, Wizara ilitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha siku 100 cha awamu ya pili ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia vyombo vya habari. Aidha, Wizara imeshiriki katika vikao kazi vilivyofanyika Dar es Salaam, Dodoma na Arusha pamoja na kufanya vikao 10 vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kujadili Sera, Kanuni, Sheria, Miongozo na Miradi mbali mbali ya maendeleo ya Wizara.

77. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Wizara imefanya jumla ya vikao 33 na Wadau wa Utalii na Mambo ya Kale wa ndani na nje ya nchi na kujadili maendeleo ya sekta hizi.

78. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Wizara, imeingia makubaliano na taasisi tofauti

zikiwemo Infinity Cultural Development kwa lengo la uendelezaji, uhifadhi na ukarabati wa maeneo ya kihistoria Zanzibar. Vile vile, katika uendelezaji wa elimu ya utalii Wizara imeingia makubaliano na Zanzibar Cable Television Limited, TUI Care Foundation na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar. Aidha, Wizara imefanya makabidhiano ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii (ZIToD) kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na kuja Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**79. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekuwa na mahusiano ya maeneo ya mashirikiano katika programu mbali mbali na wadau mbali mbali na Mashirika ya Kimataifa. Katika utekelezaji wa shughuli hizo nahususan katika kipindi hiki Wizara imepokea wageni na wadau mbalimbali kutoka nchi kama China, Korea, Japan, Qatar, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ikiwemo Dubai na Sharjah, Kenya, Marekani, Uingereza, Italia, Ujerumani, Ufaransa, Afrika ya Kusini, pamoja Mashirika kama European Union, AFD, UNESCO, UNDP, UNICEF, UNCDF, UNIDO, UNECA, World Bank, Qatar Foundation, Oman Tourism Investment Authority (OMRAN), Waandaaji wa Miss World, Miss Universe, Wanamitandao maarufu kama Mohammed Mukhaini kutoka Oman, programu za SWIOP, Team Europe Initiative, Palladium, Chuo Kikuu cha St Andrews, Royal Agricultural University,Taasisi ya National Hospitality Institute ya Oman, Chuo cha IIT-Madras Zanzibar Campus na Taasisi ya IIT Madras Global, Repro India Limited.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,371,576,420/=** na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,250,530,991.25/=** sawa na asilimia **52.73. Shilingi 1,241,844,840/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufika Machi 2026 **Shilingi 415,910,797.75/=** zilipatikana sawa na asilimia **33.49.** Vile vile **Shilingi 1,129,731,580/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 834,620,193.50/=** sawa na asilimia **73.88** ya makadirio. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1C na 1D).**

81. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

82. **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha Bajeti ya Wizara, kuandaa na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo ya Wizara.

**UTEKELEZAJI HALISI**

83. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba dhana ya Utalii Endelevu inafahamika, Idara Kwa kushirikiana na European Union imeandaa mafunzo ya utalii endelevu kwa waongozaji watalii Unguja na Pemba. Kukamilika kwa mafunzo hayo kumepelekea kuimarisha huduma za utalii zinazotolewa kwa wageni wanaotembelea Zanzibar.

**84. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika (UNECA) imeandaa mafunzo ya maafisa wa Serikali juu ya ukusanyaji wa taarifa za mchango wa utalii kwa uchumi wa Zanzibar. Mafunzo hayo yatapelekea kufanyika kwa kazi ya ukusanyaji wa taarifa wa Zanzibar nzima yatakayochambua mchango halisi wa utalii katika uchumi wa nchi.

**85. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi unafanikiwa kama ilivyopangwa, Idara imefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ambayo ni mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Mangapwani Unguja na Mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba. Utekelezaji wa mradi wa eneo la kihistoria la Mangapwani umefikia asilimia 95 na utekelezaji wa mradi wa eneo la kihistoria Ras Mkumbuu umefikia asilimia **95.** Uimarishaji wa maeneo ya kihistoria una lengo la kuhifadhi, kutunza na kuendeleza historia kwa faida ya vizazi pamoja na kuongeza vivutio vya utalii.

**86. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera, na Utafiti imetayarisha na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Malengo na Shabaha za Mpango wa Maendeleo wa ZADEP katika sekta za Utalii na Mambo ya Kale kwa Tume ya Mipango, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Pia, Idara imefanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Malengo na Shughuli zinazotekelezwa na Idara na Taasisi za Wizara.

**87. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 478,756,739/=** na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 179,120,519.52/=** sawa na asilimia **37.41**. **Shilingi 257,584,999/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufika Machi 2026 **Shilingi 50,450,857.02/=** zilipatikana sawa na asilimi**a 19.59**. Vile vile, **Shilingi 221,171,740/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara, na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 128,669,662.50/=** sawa na asilimia 58.18 ya makadirio. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D).**

**88. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

**UTEKELEZAJI HALISI**

**89. Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu Miradi ya Maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

**90. Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imefanya Utafiti mdogo wa kuangalia Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya kihistoria, utafiti huu pia ulijumuisha utoaji wa elimu juu ya mabadiliko ya Tabianchi na maeneo ya kihistoria Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba Utafiti huu ulihusisha Shehia tano ambazo ni Shehia ya Piki, Shehia ya Mtambwe

Kusini, Shehia ya Tondooni, Shehia ya Shumba Mjini na Shehia ya Tumbe Mashariki ambapo jumla ya wanajamii 68 walifikiwa wanawake 32 na wanaume 36. Kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba Utafiti ulihusisha Shehia sita ambazo ni Shehia ya Dodo, Shehia ya Kilindi, Shehia ya Ndagoni, Shehia ya Kiwani, Shehia ya Mtangani na Shehia ya Mizingani ambapo jumla ya wanajamii 104 walifikiwa wanawake 41 na wanaume 63.

91. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba inaendelea kushirikiana na wadau wa ndani kwa kufanya kongamano la wadau wa Utalii na Mambo ya Kale lililofanyika tarehe 23/01/2026 likiwa na wadau wa Utalii na Mambo ya Kale pamoja na taasisi za Serikali na Sekta Binafsi kisiwani Pemba. Aidha, Ofisi Kuu Pemba imeratibu na kufanya ufuatiliaji wa Miradi na shughuli za Wizara ikiwemo ziara mbali mbali zilizohusisha uongozi wa Wizara na taasisi nyengine zilizolenga kufanya ufuatiliaji katika Miradi ya Wizara.

92. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi kuu Pemba imeratibu ziara ya wageni kutoka Mamlaka ya Makumbusho ya Taifa Oman. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuangalia maeneo ya mashirikiano kwa upande wa Pemba. Ziara hii ilihusisha eneo la kihistoria la Chwaka Tumbe kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba katika eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu na Makumbusho ya Chake Chake. Aidha, Ofisi imeratibu vikao vya kiutendaji vya Wizara Pemba vikao vya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo, vikao vya wafanyakazi pamoja na kuandaa ripoti za utekelezaji wa Miradi ya Wizara kwa Pemba.

93. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imegharamia mafunzo kwa wafanyakazi nane, wafanyakazi wawili ngazi ya shahada ya usimamizi wa rasilimali watu na shahada ya pili ya uchumi. Wafanyakazi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ambayo ni mafunzo ya Teknolojia ya Habari (IT) na utunzaji wa Nyaraka na Kumbumbu za ofisi. Pia mafunzo ya takwimu katika ufuatiliaji na Mipango pamoja na mafunzo ya usimamizi wa data kwa kutumia excel, usimamizi wa stahiki za wafanyakazi na wastaafu yaliyotolewa na ZSSF.

94. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imewapatia wafanyakazi mafunzo kwa ajili ya kuongeza uelewa juu ya maradhi yasioambukiza pamoja na elimu juu ya Rushwa na uhujumu wa Uchumi. Jumla ya wafanyakazi 49 walipatiwa mafunzo hayo, wanawake 21 na wanaume 28. Vile vile, Ofisi Kuu imewapatia wafanyakazi mafunzo juu ya masuala ya Sheria na Kanunuzi za Utumishi Serikalini jumla ya wafanyakazi 27 walipatiwa mafunzo hayo wanawake 12 na wanaume 15.

95. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imesimamia upatikanaji wa vitendea kazi, matengenezo ya zana, vifaa vya kuandikia na huduma za uendeshaji na utawala. Aidha, Ofisi imelipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo malipo ya saa za ziada kwa walinzi, likizo kwa wafanyakazi watano pamoja na kuipatia Ofisi huduma muhimu ikiwemo malipo ya huduma ya ulinzi kwa kikosi cha KVZ, upatikanaji wa vifaa vya usafi, vifaa vya kompyuta, umeme , maji, malipo ya bima ya gari na fidia ya vipando kwa wananchi wa kijiji cha Makangale.

96. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,039,260,720/=** na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 578,158,200/=** sawa na asilimia **55.63**. **Shilingi 496,290,160/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufika Machi 2026 **Shilingi 134,709,450/=** zilipatikana sawa na asilimia **27.14.** Vile vile **Shilingi 542,970,560/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara, na hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kupata **Shilingi 443,448,750/=** sawa na asilimia 8**1.67** ya makadirio. Programu ndogo hii imetakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 10,000,000/=**, na hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **Shilingi 3,114,500/=** zimekusanywa sawa na asilimia **31.15. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1B, 1C na 1D).**

## J. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027.

97. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kutekeleza Programu ya Kuimarisha vivutio vya utalii vilivyopo nchini ili kuweza kuwavutia wageni zaidi (Fukwe na bahari, urithi wa mambo ya kale, michezo, vyakula, mikutano, halal tourism, mila na utamaduni, afya, kwa kuzingatia mashindano makubwa ya AFCON 2027 yanayokuja Tanzania na pia kuchezwa Zanzibar.

ii. Uendelezaji wa mashirikiano kati ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale na Wizara ya Mambo ya Kale na Utalii ya Oman katika ukarabati na uendelezaji wa majengo ya kihistoria ya Mji Mkongwe (Makumbusho ya Amaan, Beit el Ajaib, Beit Oman, Beit Barghash, Sultan's Palace, Grand Palace), Kasri la Mtoni na Kasri la Kibweni.
iii. Utekelezaji wa ubia (Public Private Partnership) katika ukarabati wa majengo ya kihistoria ya Mahakama Kuu ya Zamani ya Zanzibar, Ngome Kongwe, Mahamam ya Hamamni na Forodhani, Mahamam ya Kidichi na Kizimbani, Magofu ya Kihistoria ya Maruhubi, unaofanywa na Kampuni ya Infinity Cultural Development.
iv. Uimarishaji wa Eneo la Kihistoria la Fukuchani na Kampuni ya Heritage.
v. Utekelezaji wa Miradi ya Benki ya Dunia ya Big-Z Mji Mkongwe, Nungwi, Chwaka, Makunduchi, na Chake Chake, Pemba.
vi. Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Kamisheni ya Utalii ikiwemo Sea Taxi, Tourism Bazaars, Marinas, Theme Parks, Nungwi Shopping Complex, Global Village.
vii. Utekelezaji wa Miradi ya Kijamii (Community Based Tourism).
viii. Utekelezaji wa Miradi ya kuyahifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba.

ix. Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii ili kiweze kutoa huduma bora kwa mashirikiano na wadau wa maendeleo na Sekta Binafsi.

x. Kuendelea na mradi wa kuzifanyia matengenezo baadhi ya nyumba zilizopo katika hali mbaya ndani ya eneo la Mji Mkongwe.

xi. Ukondoishaji wa viwango vya mfumo wa Utalii Endelevu Duniani (Global Sustainable Tourism Standard) ikiwemo uhuishaji wa Tourism Satellite Account, Utafiti wa Athari za Kiuchumi za Sekta ya Utalii, Uwezeshaji wa wanajamii, utafiti wa matumizi ya nishati katika sekta ya utalii, mkakati wa Zanzibar Tourism Brand, utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Mageuzi katika Utalii (Tourism Transformation Plan), utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Kuifungua Pemba kiutalii (Pemba Tourism Masterplan).

## K. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**98. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepangiwa jumla ya **Shilingi 65,627,042,326/=** Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,152,300,000/=** ni kwa matumizi ya kawaida, **Shilingi 3,948,920,000/=** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 57,525,822,326/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara imepangiwa kukusanya mapato yanayokwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali **Shilingi 3,824,260,000/=.** (T**afadhali angalia kiambatisho namba 1E na 1F).**

99. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako kwamba Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar (ZIToD) kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kitasimamiwa na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Hivyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,842,610,000/=** kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo ambapo **Shilingi 1,200,000,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 642,610,000** ni kwa ajili ya mshahara na **Shilingi 1,000,000,000/=** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo.

100. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya **Shilingi 57,525,822,326/=** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na kati ya hizo **Shilingi 15,500,000,000/=** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria, **Shilingi 15,000,000,000** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa ukarabati wa nyumba hatarishi zilizomo ndani ya Mji Mkongwe, **Shilingi 11,000,000,000/=** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya kuimarisha vivutio vya Utalii na Ushirikishwa wa jamii na **Shilingi 1,000,000,000** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii (ZIToD). Aidha **Shilingi 15,025,822,326/=** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Beit el Ajaib ambazo ni ufadhili kutoka Serikali ya Oman. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F)**.

101. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Uendelezaji na Uhifadhi Mji Mkongwe inatarajia kukusanya **Shilingi 5,122,344,160/=,** ambapo kati ya hizo **Shilingi**

**1,422,344,160/=** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,700,000,000/=** ni kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1E na 1F)**.

**102.** **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii inatarajia kukusanya **Shilingi 12,975,502,753/=**, ambapo kati ya hizo **Shilingi 3,618,146,520/=** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 9,357,356,233/=** ni kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1E na 1F).**

## L. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**103.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 65,627,042,326/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano ambazo ni: -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.**(Shilingi 32,193,438,536/=)**
ii. Programu ya Kusimamia Maendeleoya Utalii. **(Shilingi 14,345,535,840/=)**
iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.**(Shilingi 3,484,100,400/=).**
iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii. **(Shilingi 9,491,402,353/=).**

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. **(Shilingi 19,088,068,950/=)**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1G)**

**104. Programu ya Kwanza:** Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe

**105. Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Programu hii ina jukumu la kuhakikisha kwamba maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale yanaendelezwa kwa kuhifadhiwa, kulindwa na kutangazwa pamoja na kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe ili uendelee kubaki kuwa urithi wa dunia kwa kutoa faida kwa kizazi cha sasa na baadae. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni Kuyaimarisha Maeneo ya Kihistoria pamoja na Kuuendeleza Mji Mkongwe. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 32,193,438,536/=**

**106. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuyahifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria kwa kuyawekea uzio na kuyaimarisha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.
ii. Kuendelea na kuimarisha jitihada za kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika maeneo ya kihistoria.
iii. Kuweka vifaa vya Makumbusho katika Makumbusho yanayoendelezwa.

iv. Kuzifanya rasilimali za historia na urithi wa utamaduni kuwa kichocheo cha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia shughuli za Utalii.
v. Uelimishwaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na Urithi wa Utamaduni.
vi. Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia Uhifadhi wa Majengo na maeneo ya Mji Mkongwe.
vii. Kuimarisha maeneo, majengo na miundombinu ndani ya Mji Mkongwe.
viii. Kuutangaza Mji Mkongwe kitaifa na kimataifa.
ix. Kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

**107. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 397,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 1,270,616,210/=** kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 30,525,822,326/=** kwa kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,500,000,000/=** ni fedha zinazotoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shilingi 15,025,822,326/= ni fedha kutoka Serikali ya Oman. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe Makusanyo ya Programu hii ya **Shilingi 3,807,260,000/=** zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Aidha, Mamlaka ya Uendelezaji na Uhifadhi Mji Mkongwe inatarajia kukusanya na kutumia S**hilingi 5,122,344,160/=**, kati ya hizo **Shilingi 1,422,344,160/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi**

**3,700,000,000/=** kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

**Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.**

**108.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii inatekelezwa na Idara ya Utalii. Jukumu la msingi katika programu hii ni Kusimamia na Kuratibu Shughuli za Utalii pamoja na kuwahamasisha wananchi juu ya dhana ya Utalii kwa Wote. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii wenye kuleta manufaa kwa wananchi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu na Uendelezaji wa shughuli za Utalii. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 14,345,535,840/=**

**109.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuviendeleza vivutio vipya vya utalii vilivyoibuliwa Unguja na Pemba.
ii. Kuratibu utendaji wa Kamati za Utalii za Wilaya pamoja na wananchi ili kuimarisha utekelezaji wa dhana ya Utalii kwa Wote.
iii. Kuimarisha utolewaji huduma za utalii ili zifikie kiwango cha juu kwa kuelimisha wadau wakiwemo wenye kuandaa misafara ya utalii, watembeza watalii, wajasiriamali wa bidhaa za utalii na waendesha mashamba ya utalii.
iv. Kuimarisha masoko ya bidhaa za kitalii za wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye mahoteli na miradi mengine ya kitalii.

v. Kuratibu ushiriki wa Zanzibar katika itifaki za kitaifa na kimataifa zinazohusiana na sekta ya utalii na masuala ya mambo ya kale ikiwemo zinazoratibiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi nyengine za kitaifa na kimataifa.
vi. Kuratibu mikutano ya wadau wa sekta ya utalii yenye lengo la kuzungumzia namna bora ya kuendesha utalii na kupunguza changamoto zilizopo kwa kushirikisha wadau wa sekta binafsi na sekta ya umma.
vii. Kuratibu na kushajiisha harakati za maendeleo endelevu ya utalii yenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira na kuimarisha usafi katika maeneo ya utalii Unguja na Pemba.

110. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 1,416,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 929,535,840/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 12,000,000,000/=** kwa kazi za Maendeleo.

**Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.**

111. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

**112. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuitangaza Zanzibar kitaifa, kikanda na kimataifa.
ii. Kuandaa na kushiriki katika maonesho, mikutano na makongamano ya utalii ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuvutia wageni kuvitembelea vivutio vya utalii vya Zanzibar.
iii. Kuandaa Tamasha la Utamaduni la Michezo (Pemba Tourists Bonanza)
iv. Kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar ipate fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.
v. Kujisajili na kushiriki katika Taasisi za Kimataifa za Mikutano (Conventions' Association)

**113. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2026/2027, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha makusanyo yatakayotumiwa na programu hii ambayo ni jumla ya **Shilingi 3,484,100,400/=** kwa kazi za kawaida.

**Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.**

**114. Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora na rasilimali watu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni

ya Utalii, ambayo itakuwa na programu ndogo mbili nazo ni: -

i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango.
ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii.

115. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango, inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala. Programu ndogo hii ina lengo la kupanga na kuimarisha uwezo wa Kamisheni ili iweze kutekeleza majukumu yake.

116. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Rasilimali Watu na Mipango inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya utafiti wa utokaji wa wageni ili kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku.
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.
iii. Kuandaa na kuendesha vikao vya Makamishna na Wadau wa Utalii
iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Kamisheni ya Utalii na Miradi ya Maendeleo.
v. Kuimarisha mahusiano baina ya Kamisheni ya Utalii na taasisi za Serikali na binafsi.

117. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2026/2027, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na programu

ndogo hii, ambayo ni **Shilingi 4,676,327,833/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 3,618,146,520/=** kwa ajili ya mishahara.

**118. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu na Shughuli za Utalii, inatekelezwa na Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii. Programu ndogo hii ina lengo la kusimamia na kuratibu maendeleo ya Utalii nchini kwa kushajiisha uwekezaji vitega uchumi katika sekta ya Utalii Zanzibar.

**119. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukagua na kufuatilia miradi ya utalii ili kuhakiki huduma zinazotolewa.
ii. Kuorodhesha idadi ya mahoteli na mikahawa ya kitalii iliyopo nchini.
iii. Kuandaa mafunzo kwa maofisa watakaofanya kazi ya kuweka viwango vya madaraja kwa bidhaa za utalii kwa vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
iv. Kukiimarisha kikosi cha Utalii na Diplomasia.

**120. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2026/2027, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na Programu ndogo hii ya **Shilingi 1,196,928,000/=** kwa kazi za kawaida.

## Programu ya Tano: Utawala na Uendeshaji

**121. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa Usimamizi Bora wa Mipango na Uendeshaji wa Rasilimali Watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 19,088,067,950/=** na itasimamia programu ndogo tatu ambazo ni: -

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. **(Shilingi 16,076,890,150/=)**.
ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. **(Shilingi 1,825,924,800 /=)**.
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. **(Shilingi 1,185,253,000/=)**.

**122. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la Kupanga, Kutayarisha, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

**123. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera na Tafiti, Kuandaa Bajeti pamoja na Kuratibu na Kusimamia Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

**124. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusimamia, Kufuatilia na Kutathimini utekelezaji wa shughuli na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.
ii. Kuratibu Vikao vya Ushirikiano kati ya SMZ na SMT kwa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.
iii. Utekelezaji wa Vipaumbele vya Ukondoishaji wa Viwango vya Utalii endelevu vya kimataifa.
iv. Kuendelea kutafuta washirika wa maendeleo watakaoshirikiana na Wizara katika kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara.

**125. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2026/2027, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 894,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 182,890,150/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 15,000,000,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**126. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la Kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi, Maendeleo, Wajibu na Maslahi ya Wafanyakazi wa Wizara.

**127. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu

wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Kujenga uwezo na Mazingira Mazuri ya Kazi kwa Wafanyakazi na Usimamizi wa Mpango wa Manunuzi na Fedha.

**128. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi.
ii. Kupima utendaji kazi wa wafanyakazi wa Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Wizara.
iii. Kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi na kusimamia utekelezaji wa Sheria mpya ya Kanuni ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na Sheria na Kanuni za Fedha.
iv. Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi wa Wizara.
v. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wadau, Taasisi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Wizara kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

**129. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2026/2027, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 800,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 1,025,924,800/=** kwa ajili ya mishahara.

130. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba, ina jukumu la Kuhakikisha kuwa Majukumu, Malengo na Shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

131. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, Kuratibu Miradi ya Maendeleo na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi na Mazingira mazuri ya kazi.

132. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba.
ii. Kushirikiana na Wadau wa Utalii katika kuifungua na kuitangaza Pemba kwenye sekta ya utalii
iii. Kuhamasisha utalii wa ndani wenye tija kwa wananchi
iv. Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Malengo na Miradi inayotekelezwa Pemba.
v. Kuratibu na kusimamia Matamasha na Matukio ya Utalii na Mambo ya Kale yatakayofanyika Pemba.
vi. Kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**133. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2026/2027, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 645,300,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 539,953,000/=** kwa ajili ya mishahara. Aidha, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe makusanyo kwa programu ndogo ya **Shilingi 17,000,000/=** zitakazoingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

## M. SHUKURANI

**134. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba hii, naomba kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kutupa Ushauri, Miongozo na Maelekezo katika kuziendeleza sekta hizi za Utalii na Mambo ya Kale kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na kuinua kipato kwa wananchi. Aidha, nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi kwa miaka mengine mitano. Nitumie fursa hii kumuomba Mwenye enzi Mungu amjaalie Rais wetu, Afya njema, Hekima, Busara na Uwezo wa kuendelea kutuongoza tena baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 na kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika kuzidi kuwaletea maendeleo.

135. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutoa shukurani za kipekee kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya misingi imara ya Muungano wetu, huku akihakikisha kwamba Taifa hili linaendelea kubakia katika hali ya Usalama na Amani, kwa kuzingatia misingi ya Umoja, Upendo na Mshikamano baina yetu. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoshiriki kuutangaza utalii wa nchi kupitia ziara zake za kikazi pamoja na kushiriki katika maonesho na makongamano tofauti yanayofanyika katika mataifa mbali mbali Duniani. Aidha, Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi kwa miaka mengine mitano, huku tukiamini kwamba ushindi wake unatokana na kazi kubwa aliyofanya ya kuleta Mapinduzi ya maendeleo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa Uwezo na Ujasiri wa kulitumikia Taifa.

136. **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee watendaji Wakuu wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Kaimu Afisa Mdhamini Ofisi Kuu Pemba, Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Mkrugenzi Idara ya Utalii, Mkurugenzi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale,

Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar (ZIToD) na Wakurugenzi wengine wote kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Vile vile, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara hii Unguja na Pemba kwa kuendelea kufanya kazi katika misingi ya Uwazi na Uwajibikaji, huku wakihakikisha kwamba Malengo na Majukumu ya Wizara yanafikiwa.

137. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale Unguja na Pemba kwa jinsi tunavyoendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha sekta hizi zinapata maendeleo makubwa na kwa haraka. Aidha, nitumie hadhira hii, kuwashukuru wamiliki wa vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa pamoja na mitandao ya kijamii, kwa kazi kubwa yenye ubora wa hali ya juu wanayoifanya ya kusaidia kuitangaza Zanzibar na vivutio vya utalii vilivyomo nchini pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria. Kufanya hivyo kunachochea kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini na kukuza pato la nchi.

138. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii ya kipekee kukishukuru Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono wakati nikitekeleza majukumu yangu.

139. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii ya kipekee kuishukuru familia yangu yote kwa kuanzia na mke wangu kwa upendo wake, kunisaidia, kunitia moyo na kunivumilia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wazazi wetu wa pande zote mbili kwa malezi yao yaliyo bora na kutuonesha njia sahihi ya maisha na upendo wao ambao ulituwezesha kufika hapa tulipo. Tunamuomba Mwenye-enzi-Mungu awajaalie maisha marefu na yenye afya na kuwaombea kwa Mungu aendelee kuzilaza roho za wazazi wetu waliotangulia mbele ya haki malazi mema peponi Amiin.

140. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nizishukuru Nchi, Mashirika na Taasisi ambazo zimeshirikiana kwa karibu na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, pamoja na wadau mbali mbali wa maendeleo katika kufanikisha kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara kupitia sekta zake mbili. Miongoni mwa nchi na jumuiya hizo ni, Umoja wa Ulaya, Oman, Falme za Kiarabu, Qatar, Morocco, Saudi Arabia, China, Japan, Uturuki, Brazil, Uholanzi, Jamhuri ya Korea, India, Uingereza, Marekani, Canada, Italia, Norway, Sweden, Finland, Denmark, Poland, Ureno, Indonesia, Jamaica, Ujerumani na Ufaransa.

141. **Mheshimiwa Spika,** naomba nizishukuru Wizara zote za SMZ na SMT ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afirika Mashariki kwa kuendelea kuitangaza Tanzania ikiwemo Zanzibar katika safu za Utalii za Kimataifa. Kipekee niwashukuru sana Mabalozi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo katika mataifa mbali mbali

na wanaoendelea kuitangaza Zanzibar kupitia Diplomasia ya Uchumi.

**142. Mheshimiwa Spika,** naomba nichukuwe fursa hii kuwashukuru Wadau wa Maendeleo wote ikiwemo Mashirika, Taasisi na Jumuiya za Kimataifa zikiwemo Benki ya Dunia, AFD, JICA, KOICA, UNESCO, UNDP, UNEP, UNIDO, UNECA, GSTC, Qatar Foundation, Tony Blair Institute (TBI), Taasisi ya Indian Institute of Information Technology Madras (IITM- Zanzibar ), TUI Foundation, National Institute of Hospitality – Oman, Oman Tourism Investment Authority, (OMRAN), Infinity Cultural Development Limited, UK Palladium, Heritage Foundation, Expertise Francais, Aidha, nizishukuru Taasisi za ndani zikiwemo ZATI, ZATO, ZATOGA, HAZ, ZNCC, NMB, CRDB, PBZ, PDB, TANAPA, Jumuiya ya Kanisa la Anglikana, Jumuiya ya "Light upon Light" ya Mufti Menki, Mwambao Coastal Community Network Tanzania, Chumbe Island Coral Park (CHICOP) na Taasisi zisizo za Kiserikali mbali mbali zinazojishughulisha na masuala ya utalii wa jamii (community based tourism).

## MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**143. Mheshimiwa Spika,** ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya Wizara ya **Shilingi 65,627,042,326/=**. Kati ya hizo **Shilingi 4,152,300,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 3,948,920,000/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi**

**57,525,822,326/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe makusanyo ya mapato ya **Shilingi 3,824,260,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

144. **Mheshimiwa Spika,** ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuidhinisha makusanyo ya **Shilingi 12,975,502,753/=** ambazo zitakusanywa na Kamisheni ya Utalii, kati ya hizo **Shilingi 3,618,146,520/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 9,357,356,233/=** kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

145. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imeruhusiwa kukusanya na kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vyake vya mapato, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe makusanyo ya **Shilingi 5,122,344,160/=.** Kati ya hizo **Shilingi 1,422,344,160/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,700,000,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## N. HITIMISHO

146. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima nainawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu Waipokee, Waijadili, Watushauri, Watuelekeze na baadae Waipitishe Bajeti hii ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**147. Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.

**Ahsante,**



**Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga (MBM),**
**Kaimu Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale,**
**Zanzibar**

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho 1A**

**MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI 2026**
**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | BAJETI 2025/2026 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 1422009 | Kiingilio cha makumbusho | 540,000,000 | 38,170,000 | 7 |
| | 1415004 | Ukodishwaji Maduka | 1,700,000,000 | 1,231,153,873 | 72 |
| Ofisi Kuu Pemba | 1422009 | Kiingilio cha Makumbusho | 10,000,000 | 3,114,500 | 31 |
| **JUMLA NDOGO** | | | **2,250,000,000** | **1,272,438,373** | **57** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | | **2,250,000,000** | **1,272,438,373** | **57** |

**MAPATO YA KAMISHENI YA UTALII YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI 2026**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | BAJETI 2025/2026 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii<br><br>Unguja | 1422025 | Leseni za biashara ya Utalii | 6,698,296,200 | 6,225,210,077.45 | 93 |
| | 1421007 | Stika na Vibali vya Mgari ya Utalii | 950,760,800 | 700,691,853 | 74 |
| | 142210 | Maombi ya Fomu Mbalimbali | 529,510,800 | 400,448,802 | 76 |
| | 142210 | Huduma za miradi | 1,902,634,869 | 1,590,112,636.93 | 84 |
| | 142210 | Vitambulisho Vya Watembeza Watalii | 300,260,800 | 211,783,904 | 71 |
| | 142210 | Faini | - | 335,752,568 | 0 |
| | 142210 | Huduma nyenginezo | 854,260,800 | 822,526,163 | 96 |
| | | Mabuku ya usajili wawageni | 214,661,600 | 64,833,500 | 30 |
| **Jumla Ndogo** | | | **11,450,385,869** | **10,351,359,504.38** | **90** |
| **pemba** | 1422025 | Leseni za biashara ya Utalii | 200,500,000 | 163,556,675 | 82 |
| | 1421007 | Stika na Vibali vya Mgari ya Utalii | 3,630,000 | 960,000,000 | 26 |
| | 142210 | Huduma za miradi | 6,600,000 | 1,971,000,000 | 30 |
| | 142210 | Mabuku ya usajili wawageni | 7,600,000 | 4,823,200 | 63 |
| **Jumla Ndogo** | | | **218,330,000** | **171,310,875** | **78** |
| **Jumla Kuu** | | | **11,668,715,869** | **10,522,670,379.38** | **90** |

**MAPATO YA MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI 2026**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | BAJETI 2025/2026 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAMLAKA YA KIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE | 14230128 | Ada ya Ukusanyaji wa taka | 360,000,000 | 653,344,000 | 181.4 |
| | 14220203 | Leseni za Biashara | 2,752,000,000 | 1,162,704,635 | 42.2 |
| | 14310101 | Faini | 180,000,000 | 283,066,818 | 157.2 |
| | 14310112 | Malipo ya matumizi ya maeneno ya wazi | 306,000,000 | 187,359,656 | 61.2 |
| | 14150113 | Kodi ya Majengo | 2,000,000 | 1,202,000 | 51 |
| **JUMLA KUU** | | | **3,600,000,000** | **2,287,677,102** | **63.5** |

**Kiambatisho 1B**

**FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Program Ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | MAPATO ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | **2,240,000,000** | 1,269,323,873 | 56.67 |
| Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe | 3,600,000,000 | 2,287,677,102 | 63.50 |
| **JUMLA** | **2,240,000,000** | **1,269,323,873** | **56.67** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | MAPATO ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara Ya Mipango) | 11,668,715,569 | 10,522,670,379 | 90.1 |
| **JUMLA** | **11,668,715,569** | **10,522,670,379** | **90.1** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | MAPATO ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 10,000,000 | 3,114,500 | 31.15 |
| **JUMLA** | **10,000,000** | **3,114,500** | **31.15** |

**Kiambatisho 1C**

**TAASISI ZISIZOPEKEA RUZUKU**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI JULAI 2025-2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI –MACHI 2025-2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | Mshahara | 542,970,560 | 443,488,750 | 81.67 |
| | M/Mengineyo | 496,290,160 | 134,709,450 | 27.14 |
| **JUMLA** | | **1,039,260,720** | **578,158,200** | **55.63** |
| **Idara ya Mipango Sera na Utafiti** | Mishahara | 221,171,740 | 128,669,662.50 | 58.18 |
| | M/Mengineyo | 257,584,999 | 50,450,857.02 | 19.59 |
| **JUMLA** | | **478,756,739** | **179,120,519.52** | **37.41** |
| **Idara ya Uendeshaji na Utumishi** | Mshahara | 1,129,731,580 | 834,620,193.50 | 73.88 |
| | M/Mengineyo | 1,241,844,840 | 415,910,797.75 | 33.49 |
| **JUMLA** | | **2,371,576,420** | **1,250,530,991.25** | **53** |
| **Idara ya Utalii** | Mshahara | 289,971,546 | 204,417,600 | 70.50 |
| | M/Mengineyo | 694,210,000 | 127,446,710.95 | 18.36 |
| **JUMLA** | | **984,181,546** | **331,864,310.95** | **33.72** |
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | Mshahara | 1,462,654,575 | 974,087,367.50 | 66.60 |
| | M/Mengineyo | 520,370,000 | 124,012,115.98 | 23.83 |
| **JUMLA** | | **1,983,024,575** | **1,098,099,483.48** | **55.37** |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,646,500,000** | **2,585,243,573.50** | **70.90** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEYO** | | **3,210,300,300** | **852,529,931.70** | **26.50** |
| **JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **6,856,800,000** | **3,437,773,505.20** | **50.11** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI JULAI 2025-2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI –MACHI 2025-2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | Mshahara | 1,149,400,000 | 811,464,331 | 70.60 |
| | M/Mengineyo | - | - | - |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **1,149,400,000** | **811,464,331** | **70.60** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEYO** | | **-** | **-** | **-** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,149,400,000** | **811,464,331** | **70.60** |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,795,900,000** | **3,396,707,904.5** | **70.83** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **3,210,300,000** | **852,529,931.70** | **26.56** |
| **JUMLA KUU YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **8,006,200,000** | **4,249,237,836.20** | **53.07** |

**MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI JULAI 2025-2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI –MACHI 2025-2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | Mshahara | - | - | - |
| | M/Mengineyo | 3,600,000,000 | 2,287,677,102 | 63.5 |
| **JUMLA NDOGO** | | **3,600,000,000** | **2,287,677,102** | **63.5** |
| **JUMLA KUU YA MAMLAKA** | | **3,600,000,000** | **2,287,677,102** | **63.5** |

**KAMISHENI YA UTALII**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI JULAI 2025-2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI –MACHI 2025-2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii** | Mshahara | 2,582,899,269 | 1,789,745,170 | 69.2 |
| | M/Mengineyo | 7,085,816,600 | 5,041,757,945 | 71.1 |
| | Mapato yanayokwenda hazina | 2,000,000,000 | - | - |
| **JUMLA NDOGO** | | **11,668,715,869** | **6,831,503,115** | **58.54** |
| **JUMLA YA MSHAHARA** | | **2,582,899,269** | **1,789,745,170** | **69.20** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO** | | **7,085,816,600** | **5,041,757,945** | **71.1** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **11,668,715,869** | **6,831,503,115** | **58.54** |

**MIRADI YA MAENDELEO**

| TAASISI | JINA LA MRADI | BAJETI JULAI 2025-2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI –MACHI 2025-2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Kuimarisha maeneo ya Kihistoria | 6,000,000,000 | 406,013,683 | 6.77 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Ukarabati wa Nyumba Hatarishi za Mji Mkongwe | 10,000,000,000 | - | - |
| | Ukarabati wa Jengo la Beit al Ajaib | 15,025,822,000 | 12,530,434,919.07 | 83.39 |
| Idara ya Utalii | Programu ya kuimarisha vivutio vya Utalii | 6,000,000,000 | - | - |
| **JUMLA KUU MIRADI YA MAENDELEO** | | **37,025,822,000** | **12,936,448,602.07** | **34.94** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **45,032,022,000** | **17,185,686,438.27** | **38.16** |

Kiambatisho 1D

**FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Program Ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | **33,008,846,575** | 14,034,548,085.55 | **42.52** |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | **1,149,400,000** | 811,464,331 | 70.60 |
| **JUMLA** | **34,158,246,575** | **14,846,012,416.55** | **43.46** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Utalii | 6,984,181,546 | 331,864,310.95 | 4.75 |
| **JUMLA** | **6,984,181,546** | **331,864,310.95** | **4.75** |

**Program ya Utangazji na Uhamasishaji Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii( Idara ya Masoko) | 1,263,753,800 | 1,731,109,954 | **137** |
| **JUMLA** | **1,263,753,800** | **1,731,109,954** | **137** |

**Program ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango na Uratibu wa Utalii) | 5,857,622,069 | 5,100,393,161 | 87.1 |
| **JUMLA** | **5,822,062,800** | **5,100,393,161** | **87.1** |

**Program Ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 2,371,576,420 | 1,250,530,991.25 | 52.73 |
| **JUMLA** | **2,371,576,420** | **1,250,530,991.25** | **52.73** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 478,756,739 | 179,120,519.52 | 37.41 |
| **JUMLA** | **478,756,739** | **179,120,519.52** | **37.41** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 1,039,260,720 | 578,158,200 | 55.63 |
| **JUMLA** | **1,039,260,720** | **578,158,200** | **55.63** |

**Kiambatisho 1E**

**MAKADIRIO YA MAPATO YA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**MAPATO YA WIZARA**

| **TAASISI** | **BAJETI 2026/2027** |
|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 3,807,260,000 |
| Ofisi Kuu Pemba | 17,000,000, |
| **JUMLA NDOGO** | **3,824,260,000** |
| Kamisheni ya Utalii | 12,975,502,753 |
| **JUMLA NDOGO** | **12,975,502,753** |
| Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe | 5,122,344,160 |
| **JUMLA NDOGO** | **5,122,344,160** |
| **JUMLA KUU** | **21,922,106,913** |

**Kiambatisho 1F**

**FEDHA INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI JULAI 2026-2027 |
|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | Mshahara | 539,953,000 |
| | M/Mengineyo | 645,300,000 |
| **JUMLA** | | **1,185,253,000** |
| **Idara ya Mipango Sera na Utafiti** | Mishahara | 182,890,150 |
| | M/Mengineyo | 894,000,000 |
| **JUMLA** | | **1,074,890,150** |
| **Idara ya Uendeshaji na Utumishi** | Mshahara | 1,025,924,800 |
| | M/Mengineyo | 800,000,000 |
| **JUMLA** | | **1,825,924,800** |
| **Idara ya Utalii** | Mshahara | 286,925,840 |
| | M/Mengineyo | 216,000,000 |
| **JUMLA** | | **502,925,840** |
| **Chuo cha Maendeleo ya Utalii** | Mshahara | 642,953,000 |
| | M/Mengineyo | 1,200,000,000 |
| **JUMLA** | | **1,842,610,000** |
| **Idara ya Makumbusho** | Mshahara | 1,270,616,210 |
| | M/Mengineyo | 397,000,000 |
| **JUMLA** | | **1,667,616,210** |
| **JUMLA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **3,948,920,000** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **4,152,300,000** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **8,101,220,000** |

**MIRADI YA MAENDELEO**

| TAASISI | JINA LA MRADI | BAJETI JULAI 2026-2027 |
|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Kuimarisha maeneo ya Kihistoria | 15,500,000,000 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Ukarabati wa Nyumba Hatarishi za Mji Mkongwe | 15,000,000,000 |
| | Ukarabati wa Jengo la Beit al Ajaib | 15,025,822,326 |
| Idara ya Utalii | Programu ya kuimarisha vivutio vya Utalii | 11,000,000,000 |
| Chuo cha Maendeleo ya Utalii (ZIToD) | Kuwa na sehemu za kutosha za kusomea ya ZIToD | 1,000,000,000 |
| **JUMLA KUU YA MIRADI YA MAENDELEO** | | **57,525,822,326** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **65,627,042,326** |

**KAMISHENI YA UTALII**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI JULAI 2026-2027 |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii | Mshahara | 3,618,146,520 |
| | M/Mengineyo | 9,357,356,233 |
| **JUMLA** | | **12,975,502,753** |
| **JUMLA YA MSHAHARA** | | **3,618,146,520** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO** | | **9,357,356,233** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **12,975,502,753** |

**MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE**

| **TAASISI** | **MAELEZO** | **BAJETI JULAI 2026-2027** |
|---|---|---|
| Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe | Mshahara | 1,422,344,160 |
| | M/Mengineyo | 3,700,000,000 |
| **JUMLA** | | **5,122,344,160** |
| **JUMLA YA MSHAHARA YA RUZUKU** | | **1,422,344,160** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO** | | **3,700,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | **5,122,344,160** |

**Kiambatisho 1G**

**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMABO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Program Ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 32,193,438,536 | 3,807,260,000 |
| **JUMLA** | **32,193,438,536** | **3,807,260,000** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Utalii | 11,493,925,840 | - |
| Chuo cha Maendeleo ya Utalii (ZIToD) | 2,842,610,000 | - |
| **JUMLA** | **14,345,535,840** | **-** |

**Program ya Utangazji na Uhamasishaji Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko) | 3,484,100,400 | - |
| **JUMLA** | **3,484,100,400** | **-** |

**Program ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango na Uratibu wa Utalii) | 8,294,474,353 | |

| | | |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii ( Idara ya Uratibu wa Utalii) | 1,196,928,000 | 12,975,502,753 |
| **JUMLA** | **9,491,402,353** | **12,975,502,753** |

**Program Ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,825,924,800 | - |
| **JUMLA** | **1,825,924,800** | |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 16,076,890,150 | - |
| **JUMLA** | **16,076,890,150** | **-** |

**Program Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI | BAJETI JULAI 2026/2027 MAPATO |
|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 1,185,253,000 | 17,000,000 |
| **JUMLA** | **1,185,253,000** | **17,000,000** |

## KIAMBATISHO 2

| OREDHA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| S/N | JINA KAMILI | JINSIA | CHUO | FANI ANAYOSOMEA |
| 1 | Nd. Hawa Sheha Haji | Mke | Harbin University of Commercial - China | Shahada ya Pili ya Uongozi wa Utalii na Hotel |
| 2 | Nd. Rukaiya Ali Abdulrahman | Mke | Harbin Institute of Technology - China | Shahada ya Pili ya Uongozi wa Kibiashara |
| 3 | Nd. Khamis Sheha Haji | Mme | Dibrugarh Universirty - India | Phd ya Anthropology |
| 4 | Nd. Mgeni Juma Khamis | Mke | Eskisehir Osmangazi University - Uturuki | Phd ya Utalii |
| 5 | Nd. Sharifa Rashid Nderema | Mke | Beijing jiaotong University - China | Shahada ya Pili ya Urban and Rural Planning |
| 6 | Nd. Saleh Omar Abdalla | Mme | Karume | Cheti cha Plumbing and pipe Fitting |
| 7 | Nd. Omar Moh'd Bakar | Mme | Karume | Cheti cha Plumbing and pipe Fitting |
| 8 | Nd. Mudathir Mohd Ayoub | Mme | State University of Zanzibar (SUZA) | Stashahada ICT |
| 9 | Nd. Said Juma Machano | Mme | Chuo Kikuu Huria | Shahda ya Pili Tourism Planning and Management |
| 10 | Nd. Sauda Kibuda Moh'd | Mke | Kampala University Uganda | Shahada ya Kwanza Utunzaji Kumbukumbu |
| 11 | Nd. Mwaka Khamis Omar | Mke | Kampala University Uganda | Shahada ya Kwanza Business Administration |
| 12 | Nd. Saleh Juma Makame | Mme | Tanzania Institute of Accountancy (TIA) | Shahada ya Pili HR with IT |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13 | Nd. Shehe Ali Salum | Mme | University of Dar es Saalam | Shahada ya Pili Utunzaji Kumbukumbu |
| 14 | Nd. Hamad Rajab Hamad | Mme | State University of Zanzibar (SUZA) | Shahada ya Pili ya Heritage Management and Marketing |
| 15 | Nd. Hamzia Khamis Khalfan | M'ke | Kampala University Uganda | Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Rasilimali watu |
| 16 | Nd. Fatma Asaa Sharif | M'ke | Mount Kenya | Shahada ya Kwanza ya Rasilimali Watu |
| 17 | Nd. Abdalla Omar Khalifa | M'me | Yunnan University- China | Shahada ya Pili ya Economics |
| 18 | Nd. Ame Mrisho Hilal | Mme | Micro Teaching | Cheti cha ICT |
| 19 | Nd.Hafidha Mussa Shaaban | Mke | State University of Zanzibar (SUZA) | Shahada ya Kwanza Historia na Akiolojia |
| 20 | Nd. Asha Juma Nyendo | Mke | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere | Stashahada ya Uchumi (Economics) |
| 21 | Nd. Abubakar Haji Bakar | Mme | Kampala University Uganda | Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Rasilimali watu |
| 22 | Nd. Bakar Juma Othman | Mme | Mugla Sitki Kocman University Uturuki | Shahada ya Pili Akiolojia |
| 23 | Nd. Hanifa Dhamir Simai | Mke | Kampala University Uganda | Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Rasilimali watu |
| 24 | Nd. Maulid Khamis Foum | Mme | Iringa University | Shahada ya Uzamili Marketing |
| 25 | Nd. Abdulla Omar Khalifa | Mme | Yunnan University | Shahada ya Uzamili Project Management |
| 26 | Nd. Dalila Saleh Abdulla | Mke | Zanzibar University | Shahada ya Kwanza Record and Archives Management |
| 27 | Samir Hadad Khamis | Mme | Tianjin University - China | Shahada ya Uzamivu ya Usanifu Majengo |